epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumanne Novemba 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581872

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

## RIPOTI MAALUMU

**KISIWANI UZI KULIVYO...**

# Tiba mwisho alasiri, mikasa kujifungua ndani ya boti, gari

- **Kina** wakazi 4,200, mwokozi wao ni tabibu wa jadi... *Endelea ukurasa 4 & 5*




Jengo la Kituo cha Afya Uzi, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, ambacho huduma hazitolewi wikiendi.

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

**WATU TISA WAFA BAADA YA MAKAZI KUSOMBWA NA MAJI**

## Samia: Nyumba za ibada zijenge imani, si ngome ya vurugu

UKURASA 2

**LICHA YA ZUIO LA BOT**

## Mikopo umiza mtandaoni yashika kasi

UKURASA 3



UKURASA WA 2

**Waziri** Kabudi aibuka na angalizo lake hukumu umri wa kuoa, kuolewa

UKURASA WA 18

KESI YA KUCHOMA MKE

**Ripoti** za ugonjwa wa akili zazua utata mahakamani

UKURASA WA 19

**Mbinu** mpya uuzaji 'unga', wakala wao waganga kienyeji, nyumba za kupanga

**MICHEZO** RAMOVIC ATAJA MFUMO YANGA KUIMALIZA AL HILAL UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo ya ujenzi wa Msikiti wa Al Ghaith katika eneo la Kilakala Flats, mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

# Samia: Dini ni sehemu pekee kujenga jamii yenye maadili

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuwa dini zina sehemu muhimu na ya kipekee katika kuendelea kujenga jamii yenye maadili, umoja, upendo, amani na mshikamano.

Pia amewakumbusha waumini wa dini ya Kiislam kuendelea kujenga madrasa nyingi zaidi, ili kuwapatia watoto mafunzo ya kiimani yatakayowawezesha kuwa raia wema na waadilifu kwa familia na taifa kwa ujumla.

Amewataka waumini wa madhehebu ya dini kutumia nyumba za ibada kujijenga kiimani badala ya kuzitumia kama chanzo cha vurugu na uvunjifu wa amani.

Rais Samia alisema hayo mjini Morogoro baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa Msikiti wa Al Ghaith unaotajwa kuwa mkubwa wa kwanza kwa Afrika Mashariki ulio chini ya Taasisi ya Islam Foundation unaofadhiliwa na Jumuiya ya Dar al ber Society ya Dubai kutoka nchi ya Falme za Kiarabu na ukikamilika utagharimu shilingi bilioni saba.

"Ni vyema nyumba hizi za ibada zikatumika kuunganisha kamba ya waumini na sio kukata kamba hiyo inayounganishwa na Mungu, mkajiita ni viongozi wa dini wakati huo huo mnasababisha mifarakano kwa waumini wenu, msifike huko mjue binadamu huwa wanatofautiana," alisema Rais Samia.

Aidha, alisema katika maeneo mengine nyumba za ibada zinazojengwa badala ya kuleta neema na kuwafanya waumini kuabudu na kupata heri kwa pamoja wengine wamekuwa wakizigeuza chanzo cha vurugu.

Katika hatua nyingine, Rais Samia akitumia kusanyiko hilo kuwafunda wanawake kwenye jukumu la malezi kwa watoto ili kupunguza ama kumaliza changamoto ya mmomonyoko wa maadili unaoendelea badala ya jukumu hilo kuwaachia wanaume.

Aidha, aliwaasa kinamama kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya malezi ya watoto badala ya kutegemea kinababa ambao ndio wamekuwa wakiogopwa na watoto kwa sasa kwa kuwa mtoto anapokosea badala ya mama kukaa naye chini na kumfundisha humtishia kuyafikisha kwa baba yake.

"Mama anamwambia mtoto kila nikikwambia husikii sasa ngoja baba ako aje, kwa nini umtishie baba na kwanini wewe mama usisimame kama wewe kwa kutumia lugha nzuri na kumwelewesha mtoto na akakuelewa? Kinamama mkaze kamba katika suala zima la malezi yanayofaa ambayo yanakwenda sambamba na imani kwa kusimamia misingi ya malezi bora kwa watoto wenu," alisisitiza Samia. Pamoja na kupongeza Taasisi ya Islamic Foundation kujenga misikiti zaidi ya 1,000 nchini, aliwahimiza ujenzi wa madrasa za kutosha ili zisaidie kutoa elimu kwa watoto na kuwa na jamii yenye maadili mema na kumjua Mungu.

Aliipongeza taasisi hiyo pia kuendelea kutoa michango yake kwenye jamii hususani kwenye sekta za afya, elimu na maji na kwamba hatua hiyo ni sadaka nzuri inayoishi wakati wote kwa kuwa huduma hizo ni muhimu kwenye jamii.

Awali, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, alimpongeza Rais Samia kwa kuwa mstari wa mbele kushiriki matukio anayoalikwa na taasisi za dini.

Alisema pamoja na serikali kusimamia vyombo vya ulinzi na usalama katika suala zima la kulinda amani na utulivu, taasisi hizo za dini zina mchango mkubwa katika kulinda amani na utulivu.

"Lakini baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitumia kipindi hiki cha uchaguzi kushawishi wananchi kujiingiza katika vurugu na kusababisha uvunjifu wa amani ni vyema mkajiepusha na hali hiyo ili kuendelea kufaidi matunda ya amani na utulivu uliopo," alisema Waziri Masauni.

Naye Rais wa Taasisi ya Islamic Foundation, Arif Nahad, alisema mradi huo wa msikiti ulianza kujengwa Oktoba, 2021 na sasa umefikia asilimia 80 ya utekelezaji ambao ukikamilika utawezesha kuwapokea waumini 3,000 kwa wakati mmoja na huduma nyingine kama eneo la kuhifadhia na kuosha maiti, maktaba ya kisasa, nyumba za kupumzikia mashehe pamoja na madrasa.

"Taasisi hii imefanikiwa kujenga misikiti zaidi ya 1,600 katika maeneo mbalimbali kwa Tanzania Bara na Visiwani na misikiti hiyo ina madrasa zenye wanafunzi takribani 80,000.

"Tumekuwa pia tunatoa huduma ya majisafi na salama kwa jamii kwa kuchimba visima virefu na vifupi ambapo kwa sasa tumefanikiwa kuchimba visima zaidi ya 3,000 kwenye maeneo mbalimbali Tanzania bara na visiwani," alisema Nahad.

Alimwomba Rais Samia kuisaidia taasisi hiyo kufanikisha ujenzi wa chuo cha ualimu na maadili katika eneo lake lenye ekari zaidi ya 38 lililoko Kitungwa wilayani Morogoro, ombi ambalo Rais aliridhia.

Rais Samia amemaliza ziara yake ya siku mbili mkoani Morogoro na kuelekea mkoani Dodoma.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Kabudi aibuka na angalizo hukumu umri wa kuolewa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, ametoa angalizo kwamba kifungu kilichotumika katika kesi ya umri wa kuoa na kuolewa iliyofunguliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, hakikuwa sahihi.

Prof. Kabudi alitoa kauli hiyo jana Dar es Salaam wakati akifungua kampeni ya siku 16 za uanaharakati wa kupinga ukatili wa kijinsia iliyojumuisha wadau wa Mtandao wa Kupinga Ukatili (MKUKI) chini ya uratibu wa Shirika la Wanawake na Maendeleo Afrika (WiLDAF).

"Lakini niseme, kwa sisi wanasheria wa Tanzania tumeanza kusahau mfumo wetu wa sheria, sisi tunatumia The English Common Law System. Uamuzi wa mahakama ni sehemu ya sheria zetu, hasa ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

"Lakini makosa hayo si yenu, makosa hayo ni ya sisi wasomi, sisi wanataaluma, hatujaandika 'commentary' ya Katiba yetu kama walivyofanya wenzetu wa India, ndio maana kila mtu anapoisoma Katiba anaisoma ilivyo. Inabidi tuandike 'commentary' ya Katiba, kwamba kila kwenye kifungu cha Katiba tuweke uamuzi wa mahakama.

"Na ndio maana ile kesi ya Gyumi... mimi kwa maoni yangu, kifungu kilichotumika hakikuwa sahihi, ningekuwa mimi, nisingetumia ibara ya 13 na nilisema bungeni watu hawakunielewa," alisema Prof. Kabudi.

Gyumi alifungua shauri Mahakama Kuu ya Tanzania kwa niaba ya watoto wote walio katika hatari ya kuingia katika ndoa za utotoni dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwaka 2016, kupinga uhalali wa kikatiba wa ndoa za utotoni.

Rebecca alishinda shauri hilo baada ya mahakama hiyo kutamka kwamba vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ni vya kibaguzi na vinakwenda kinyume cha Katiba na kwamba vimepitwa na wakati.

Alipinga vifungu hivyo vya 13 na 17 kwa msingi kwamba vinakiuka ibara ya 12(1) ya Katiba ya Tanzania inayotoa usawa kwa watu wote.

Pia alipinga kwamba vifungu hivyo vinakiuka ibara ya 13(1) na (2) vya Katiba hiyo ya nchi ambayo inawalinda watu dhidi ya ubaguzi kwa misingi ya kijinsia.

Alidai vifungu hivyo vya sheria pia vinakiuka ibara ya 21(2) ya Katiba hiyo kwa kutowapa wasichana fursa ya kushiriki kikamilifu katika kuamua mustakabali wa maisha yao na kwamba vinamnyima mtoto haki ya kupata elimu na uhuru wa mawazo.

HUKUMU YA KESI

Mahakama Kuu Julai 8, 2016, ilitoa hukumu ikitamka kuwa, ndoa yoyote ya mtu mwenye umri chini ya miaka 18 ni kinyume cha sheria na kwamba vifungu hivyo vinaruhusu watoto kuingia katika ndoa wakati haifai kuwaingiza watoto katika majukumu makubwa ya ndoa na kuonesha hatari zake kiafya inayowakabili watoto hao pale wanapoolewa wakiwa na umri mdogo.

Mahakama ilitoa uamuzi kwamba vifungu hivyo havitoi usawa kwa msichana na mvulana katika njia mbili; kwanza umri wa ndoa tofauti kati yao na pili, wasichana chini ya umri wa miaka 18 wanahitaji ridhaa ya wazazi kuolewa wakati wavulana hawahitaji na kuonesha kwamba tofauti hiyo inatoa maana kwamba wasichana na wavulana hawatendewi sawa chini ya vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa na kuonesha ubaguzi na vinakiuka ibara ya 12 na 13 za Katiba ya nchi.

Hata hivyo, serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu ilikata rufani kupitia hukumu hiyo namba 204 la mwaka 2017 kupinga uamuzi huo wa Mahakama Kuu lakini mwaka 2019 Mahakama ya Rufani ilimpatia tena ushindi Rebeca na kutoa mwaka mmoja sheria hiyo iwe imefanyiwa marekebisho. Lakini hadi leo serikali haijatekeleza amri ya mahakama.

LICHA YA ZUIO LA BoT

# Mikopo umiza mtandaoni yashika kasi

**Na Waandishi Wetu**

SIKU tano baada ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutangaza orodha ya programu tumizi (applications) 69 ambazo haziruhusiwi kutoa huduma ya mikopo mtandano, baadhi zimeendelea kutoa huduma hiyo huku matangazo yake yaliyodhaminiwa katika mitandao ya kijamii ya Facebook na Instagram yakishika kasi.

Hivi sasa kila aliyepakua programu tumizi ya mkopo, anakutana na matangazo katika mitandao ya kijamii yakihamasisha kuchukua mkopo, wakijinasibu kuwa "masharti yao ni rahisi na unapatikana kwa muda mfupi".

Mwandishi amebaini matangazo hayo yamelipiwa ili yasambazwe kwa kila anayeweka taarifa au kutembelea mtandao wa kijamii na ambaye alipakua programu tumizi yoyote ya mkopo.

Vilevile, mwandishi wa habari hii ametembelea programu tumizi mojawapo na kuomba mkopo ambapo alipewa maelekezo ya kurejesha fedha hizo kwa lipa namba, ilhali programu hiyo ni miongoni mwa 69 zilizotangazwa kutotambuliwa na BoT siku tano zilizopita.

"Taarifa za akaunti zetu: Tafadhali kumbuka zifuatazo ni akaunti zetu rasmi za malipo. Ili kulinda usalama wa fedha zako, tafadhali tumia akaunti rasmi kwa ajili ya malipo. Airtel 540540; Vodacom 500555; Tigo 500555; na HaloPesa 500555."

Matangazo hayo mengi yanaeleza riba ya mkopo ni asilimia moja, muda wa mkopo ni siku 180 na kiasi ambacho mtu anaweza kukopa ni Sh. 500,000 hadi milioni moja, na hawaangalii historia ya mkopo.

Pia wanaeleza kwa picha mjongeo ambazo wasichana na wavulana wanatumika kueleza namna walivyojipatia mikopo, wakishawishi kuwa wamepata mikopo yao ndani ya dakika tatu tu. Kila tangazo wameambatanisha na link ya kubonyeza ili kupakua programu tumizi husika.

Jana mwandishi alitembelea programu tumizi kadhaa na kubaini bado wanahitaji taarifa binafsi za mkopaji, ikiwamo kuona picha zake kwenye kifaa chake, kuona namba za simu alizohifadhi, kuona ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) na kwamba bila kukubali masharti husika, hawezi kupewa mkopo.

"Hakuna uchaguzi wa kitambulisho, hakuna dhamana inayohitajika, hakuna ukaguzi wa mkopo. Unaweza kukopa hadi TZS 1,000,000 kwa dakika tatu tu," ilielezwa katika moja ya matangazo hayo.

Katika moja ya matangazo, mwananchi mmoja aliweka ujumbe aliotumiwa baada ya kuchukua mkopo na muda wa kulipa haujafika. Unasomeka:

"Ukiwa kama mtu mzima mwenye meno 32 na akili timamu, sijaona sababu ya wewe kukaa kimya mpaka sasa na kuzima simu ikiwa pesa zetu ulizifuata mwenyewe kwa dhiki ulizonazo na hakuna aliyekuita na uliona kuwa leo umepitiliza muda na bado unakaza mishipa ya fahamu, hutaki kulipa.

"Sasa una saa moja ya kukamilisha malipo yako ya ZIMACASH kabla kila mtu kwenye simu yako hajaanza kupata ujumbe wa udhalilishaji kutoka kwetu na kila mtu atajua kuwa umekopa ZIMACASH, jipange!"

Mwandishi wa habari hizi alifanya uchunguzi wa miezi minne na kubaini wakopeshaji wasiofuata utaratibu na wasiotambuliwa na BoT, huwadhalilisha na kuingilia taarifa binafsi za wakopaji.

BoT ilitoa mwongozo wa wakopeshaji mtandaoni, ikiwapa siku 14 kuwasilisha maombi yao, lakini kati ya waombaji 16 waliojitokeza ni wanne pekee waliokidhi vigezo hadi Novemba 21 mwaka huu taasisi hiyo ilipotoa orodha ya wakopaji wasiotambuliwa na kuitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuzifunga programu tumizi wanazofungua.

**PDPC YAONYA**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa binafsi (PDPC) imewaonya wakopeshaji dhidi ya matumizi ya taarifa binafsi.

Jana, Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dk. Emmanuel Mkilia, alionya taasisi za mikopo zinazotoa taarifa za watu mitandaoni, akizitaka kuacha tabia hiyo mara moja, kwa kuwa watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Vilevile, alisema kuwa hadi kufikia mwezi huu, zaidi ya taasisi 700 za ukusanyaji na uchakataji taarifa binafsi nchini zimesajiliwa na tume hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi za mikopo mitandaoni hazipaswi kutoa taarifa binafsi za waliokopa kwa kuwa hilo ni kosa kisheria na wakibainika watachukuliwa hatua kali.

"Tume inawaalika wananchi wote kutoa taarifa kuhusu watu au taasisi zinazotoa taarifa zao bila ridhaa yao kwa sababu kuna sheria ya kulinda faragha za watu," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa tatizo la kuvuja kwa taarifa hizo binafsi limekuwa na madhara makubwa kwa jamii, ikiwamo kusababisha baadhi ya watu kujitoa uhai wao.

Mkurugenzi huyo alisema ipo Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya Mwaka 2022 na kanuni zake ambazo zilitungwa kwa lengo la kulinda faragha ya watu.

Alisema mazingira ya kidijitali yameleta mabadiliko makubwa katika maisha ya kila siku na kusababisha taarifa binafsi na faragha za watu kuvujishwa.

Alisema tume hiyo itaendesha warsha inayotarajiwa kufanyika Dar es Salaam kwa makundi mbalimbali kuhusu ulinzi wa taarifa hizo binafsi.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# CCM yatamba kufunga kampeni kwa kishindo

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetangaza kufunga Kampeni za Serikali za Mitaa leo kwa kishindo. Kimesema watanzania watashuhudia mabadiliko kwa sababu CCM imejipanga kushinda uchaguzi huo.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa chama hicho, Amos Makalla, aliyasema hayo jana wakati wa kampeni zilizofanyika jimbo la Kinondoni, Dar es Salaam.

Alisema kuwa wakati wa ufunguzi wa kampeni, CCM ilisambaza viongozi wake katika mikoa mbalimbali na wakati wa kuzifunga leo watabadilishana, yeye anakwenda Morogoro aliko Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika na Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi atakwenda Dar es Salaam.

Makalla alijigamba kwamba katika siku sita za kampeni Mkoa wa Dar es Salaam, viongozi wa taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) hawajaonekana mkoani humo.

"Siku zote sita sijaona kiongozi yeyote wa CHADEMA Dar es Salaam, tunatamba tu nimemwona (Freeman) Mbowe kaenda Songwe na Mbeya jana (juzi), nimemsikia akisema katika siku moja iliyobaki na mimi ninakwenda kwangu Machame (Kilimanjaro) kujitetea'. Tundu Lissu yeye mwisho ni Ikungi," alirusha kijembe kwa wanasiasa wenzake.

Makalla alisema CHADEMA hawajajiandaa kwa uchaguzi huo, akiwananga kuwa walipopewa fursa ya kutekeleza 4R, kipaumbele chao kikawa maandamano wakati CCM viongozi wake kuanzia chini hadi juu walikuwa kwa wananchi kuwaandaa kwa uchaguzi na kutatua kero zao.

Alisema mikutano yote aliyohudhuria mpaka sasa inatoa taswira na mwelekeo wa ushindi CCM.

Alisema kuwa juzi alikuwa Ukonga. Licha ya jua kali, mkutano ulikuwa mkubwa.

"Hakika kwa siku hizi sita Dar es Salaam kwetu ni siku sita za moto. Kampeni zimekuwa za kishindo na zinavyoendelea CCM itapata ushindi wa kishindo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Abbas Mtemvu, alisema wenyeviti wao wakiingia keshokutwa wanadunda miaka mitano.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Zainab Khamis Shomari (MNEC), alikishukuru chama chake kwa kuwarejeshea wagombea imara.

"Shida ya watanzania ni maendeleo ambayo yamefanyika, ndio maana tukipita katika mikutano ya wenzetu tunashangaa ni mikutano au wanafanya shooting," alidai.

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Rehema Sombi, alisema kwa kutambua vijana ndio vuguvugu la maendeleo wapo kazini kuhakikisha vijana wote wanashinda kwa kishindo kesho.




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

KISIWA CHA UZI:

# Kina kituo cha afya chenye daktari na mkunga mmoja, wakazi 4,200

- Huduma mwisho alasiri, wikiendi hakuna
- Mikasa; kujifungulia ndani ya boti, gari
- Mkunga wa jadi ndiye anaokoa jahazi lao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KWA Zanzibar, serikali inajivunia kufikia lengo la kuwa na kituo cha kutolea huduma za afya kila baada ya umbali kilomita tano.

Hata hivyo, upatikanaji huduma za afya katika vituo hivyo ni si wa uhakika, mwandishi wa habari hizi anaripoti kinachojiri visiwani katika wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Katika Kisiwa cha Uzi wilayani humo, kuna shehia mbili zenye wakazi 4,233. Hizo ni Uzi yenye 3,075 (wanawake 1,510 na wanaume 1,565) na Ng'ambwa yenye wakazi 1,158 (wanawake 571 na wanaume 587). Wote wanategemea Kituo cha Afya Uzi kupata huduma za afya.

Ni kituo kinachotoa huduma za matibabu muda saa za kazi tu; kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa). Wikiendi hakuna huduma inayotolewa kituoni huko.

Uzi ni miongoni mwa visiwa 52 vinavyoizunguka Zanzibar (saba vinakaliwa na watu vikiwa na huduma muhimu kama vile umeme, maji na vituo vya afya).

Kilio kikubwa cha wakazi wa kisiwani Uzi ni kukosekana watoa huduma za uzazi, jambo wanalolitaja linaweka hatarini uhai wa mama na mtoto.

Zahra Muhamed Muazini (26), mkazi wa kisiwa hicho, almanusura apoteze uhai baada ya kujifungua akiwa katika boti saa nane usiku wakati akipelekwa kupata huduma nje ya kisiwa hicho.

"Ninakumbuka ilikuwa Januari mwaka huu, saa nane usiku, uchungu umenikaza, kituo chetu cha afya hakifanyi kazi kwa muda huo lakini pia hakina daktari wa huduma ya mama kujifungua," anasimulia Zahra.

Mama huyo wa watoto wanne anaendelea: "Wakati uchungu umekaza, maji ya bahari nayo yameshafungamana kisiwani, huwezi kutumia mtumbwi wa kawaida kutoka nje ya kisiwa, lazima utumie usafiri wa boti.

"Usafiri unaotumika kisiwani hapa ni gari au bodaboda (pikipiki) kwa nyakati ambazo maji ya bahari hayajaingia kisiwani na kufunga barabara. Kutoka hapa Uzi hadi kijiji cha Unguja Ukuu ni wastani wa kilomita tatu.



Mwonekano wa barabara yenye urefu wa kilomita mbili kutoka Unguja Ukuu hadi Uzi ambayo maji yanapojaa, huifunika na hivyo wananchi hulazimika kutumia boti.

"Gharama za usafiri wa boti ni Sh. 1,500 kwa kila abiria, lakini nyakati za dharura, mfano wa kumsafirisha mjamzito kwa boti ni Sh. 30,000 na ni mwendo wa dakika 10 unaotumika kutoka hapa Uzi hadi Unguja Ukuu kwa usafiri wa boti."

Zahra anasema kuwa wakiwa katikati ya bahari, akipelekwa Kituo cha Afya Unguja Ukuu, alijifungua chini ya usimamizi wa mkunga wa jadi aliyemsindikiza.

"Wakati ninatoka nyumbani kwangu, niliongozana na baadhi ya wanafamilia pamoja na mkunga wa jadi ambaye hutusaidia kutuzalisha wakati wa dharura hapa kisiwani.

"Ni jambo la kusikitisha kwamba, kisiwa cha Uzi kina kituo cha afya kizuri, chenye vifaa tiba, lakini hakina wataalamu wa huduma za uzazi.

"Hii kero inatukwaza na kutudhalilisha sisi wanawake kwa sababu wakati wa kujifungua kunahitaji faragha chini ya usimamizi wa wataalamu wa afya.

"Kwa kweli siku ile sitoisahau maishani mwangu, kujifungua katika boti! Lakini ninamshukuru Mungu alinisaidia nikajifungua salama mtoto wangu wa kike ambaye hivi sasa anakaribia kutimiza umri wa mwaka mmoja," anasema Zahra.

Rai yake kwa serikali ni kuwapatia wataalamu wa afya ya uzazi ili kinamama wajifungue katika Kituo cha Afya Uzi na kuokoa maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Mkasa wa Zahra unafanana na wa Ada Sheha (30), mama wa watoto sita na mkazi wa kisiwa hicho aliyejifungua ndani ya gari wakati akiwahishwa Hospitali ya Unguja Ukuu nje ya kisiwa hicho.

"Mwaka jana (2023), nikiwa na ujauzito wa mtoto wangu wa tano, nilijifungua ndani ya gari mchana kweupe baada ya kukosa wataalamu wa afya katika Kituo cha Afya Uzi.

"Wakazi wa kisiwa hiki wanapobeba ujauzito huwa na hofu kutokana na kituo kutokuwa na wataalamu wa uzazi, hivyo baadhi hulazimika kuyahama makazi yao wanapokaribia kujifungua kwa kwenda kuishi kwa ndugu na jamaa nje ya kisiwa hiki.

"Mimi mimba zangu zote nimejifungua kwa wakunga wa jadi hapa kisiwani. Hii mimba yangu ya mtoto wa tano nilitaka nijifungulie hospitalini kwa sababu wakunga wa jadi sasa wamekatazwa kuzalisha, lakini sikufika hospitalini, nikajifungua ndani ya gari.

"Nilibahatika kuzaa mtoto wa kiume ambaye ni huyu hapa unayemwona," anasema mama huyo huku akimwonesha mwandishi mtoto wake wa tano na mwingine mchanga wa kike anayemtaja amejifungulia kwa mkunga wa jadi kisiwani huko miezi mitano iliyopita.

Ada anaungana na mwanamama mwenzake Zahra kupaza sauti dhidi ya ukosefu wa watoa huduma za uzazi kisiwani kwao, akiomba serikali ipeleke watumishi wa kutosha katika kituo hicho ili wananchi wasisumbuke.

Ramadhan Haidari (43), baba wa watoto watano katika kisiwa hicho, anasema kituo chao kina daktari mmoja, hivyo wanahitaji wataalamu wa afya wa kutosha na wawapo kituoni muda wote ili wake zao wasijifungulie kwa wakunga wa jadi.

"Tatizo hili haliwaumizi wanawake tu, hata sisi wanaume linatuumiza, tunapata tabu sana katika kupata huduma. Mimi binafsi nilikwenda na mke wangu katika kituo hicho ili apate huduma ya kujifungua lakini kutokana na kituo kutokuwa na wataalamu wa uzazi, nilimsafirisha kumpeleka Kituo cha Afya Unguja Ukuu, ile tunafika tu, akajifungua.

"Kama tungechelewa kidogo tu kumfikisha Kituo cha Afya Unguja Ukuu, angejifungulia njiani. Kama hatuna wataalamu wa afya, ninafikiri serikali iendelee kuwapa fursa wakunga wa jadi kuzalisha ili kuwasaidia wajawazito kisiwani kwetu," anasema Haidari.

**MKUNGA WA JADI**

Mtoro Ali Hassan (56), mkunga wa jadi kisiwani Uzi, anasema serikali imepiga marufuku wakunga wa jadi kuzalisha na badala yake wawaongoze wazazi kwenda kujifungua kituo cha afya.

Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa watoa huduma za afya kisiwani Uzi, Mtoro anasema hulazimika kuwasaidia kinamama kujifungua hasa nyakati za dharura.

"Ni mimi niliyemdhalilisha Zahra Muhamed Muazini tukiwa katika boti wakati akiwahishwa Kituo cha Afya Unguja Ukuu. Nililazimika kutoa msaada ili kuokoa uhai wake na mtoto, na siku hiyo ilikuwa



Zahra Muhamed Muazini aliyejifungulia katika boti wakati akiwahishwa hospitalini, akizungumza na mwandishi wa Nipashe (hayupo pichani) aliyefika nyumbani kwa mama huyo kisiwani Uzi hivi karibuni. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

**Inaendelea Ukurasa 5**

KISIWA CHA UZI:

# Kina kituo cha afya chenye daktari na mkunga mmoja, wakazi 4,200

**Inatoka Ukurasa 4**

ngumu kwangu maana sikuwa na zana yoyote," anasimulia mkunga wa jadi.

Mkunga wa jadi huyo anasema kisiwa hicho kimezungukwa na bahari, hivyo kinahitaji kuwa na huduma muhimu, zikiwamo za afya kwa saa zote 24 kwa siku zote za wiki. Wataalamu wa afya wawapo kisiwani muda wote.

"Uzazi hivi sasa ni mgumu, wakati mwingine anakuja mzazi nyakati za usiku anahitaji msaada, lakini hana zana yoyote ya kutumia kwa ajili ya kujikinga na maradhi, ninalazimika kutumia zana za kijadi, zikiwamo khanga ili kuwahudumia wanawake wenzangu," alisema mkunga huyo anayejitambulisha alianza kazi hiyo miaka 20 iliyopita.

Mkunga wa Jadi Mtoro anaomba Wizara ya Afya kuwashirikisha wakunga wa jadi ili kuwasaidia wananchi, hasa wanaoishi visiwani ambao wanakabiliwa na changamoto kupata usafiri wa baharini.

Anasema kuwa licha ya serikali kukataza wakunga wa jadi kuzalisha, baadhi ya wananchi wakaadi. Hukaa nyumbani mpaka uchungu unapokaza, hivyo kuwa vigumu kwao kukifikia kituo cha afya, hata kuangukia mikononi mwa wakunga wa jadi kupata msaada.

"Ninaungana na serikali kwamba uzazi wa sasa ni mgumu kulinganishwa na zamani kutokana na matatizo mbalimbali ya kiafya, hivyo ni sahihi kabisa wajawazito wakajifungulie hospitalini, lakini panapohitajika msaada wa dharura, tupo tayari kusaidia," anahitimisha Mtoro.

**UONGOZI WA SHEHIA**

Othman Mwinyi Haji, Sheha wa Shehia ya Uzi, anakiri kuwapo changamoto ya wataalamu wa afya katika Kituo cha Afya Uzi, akisema: "Kituo chetu cha afya ni kizuri mno, tumejengewa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Kina vifaa tiba vinavyohitajika na tena tuna mpaka nyumba za kuishi madakrati, lakini kituo hakitoi huduma kwa saa 24.

"Nyumba za madaktari zilizoko hawaishi na hao wachache waliopo katika kituo chetu cha afya wanakuja na kuondoka. Changamoto hii tumeshaiwasilisha katika ngazi za juu serikalini, wananchi kuendelea kuvumilia, serikali itatatua changamoto hii.

"Nyakati za usiku wananchi wa kisiwa hii, hasa wajawazito wanapata shida kutafuta huduma za afya na wakati mwingine hulazimika kujifungulia njiani kabla ya kufikishwa hospitalini au kujifungulia kwa wakunga wa jadi, jambo ambalo ni hatari kwa afya ya mama na mtoto."

**WASIMAMIZI WA KITUO**

Daktari Dhamana wa Kituo cha Afya Uzi, Seleh Nila Ali, anasema changamoto iliyopo ni uhaba wa wafanyakazi, hasa kwa wakunga. Kituo hicho kina mkunga mmoja na kutokana na uhaba wa wataalamu wa afya kinashindwa kuwazalisha wajawazito.

Anabainisha kuwa kwa mwezi kituo kinatoa huduma kwa wastani wa watu 500 wanaofika kupata huduma. Kati yao, watoto ni 100 na wajawazito 60 ambao hufuata huduma za awali, ikiwamo kuangalia maendeleo ya mtoto tumboni (kliniki).

Daktari huyo anasema kituo kina upungufu wa wakunga watano na madaktari watatu ili kukidhi mahitaji ya kutoa huduma za afya. Anaitaja kero hiyo ni kiini kinamama kisiwani huko kujifungulia kwa wakunga wa jadi.

"Rai yangu kwa wananchi wa kisiwa hiki ni kuhamasisha watoto wao kusoma masomo ya sayansi ili kupata wataalamu wa afya wazawa katika kisiwa hiki kwa sababu watu kutoka nje ya kisiwa hiki wanakuwa wagumu kuja kufanya kazi huku kutokana na changamoto ya usafiri," anasema.

Daktari Dhamana wa Wilaya ya Kati Unguja (DMO), Dk. Amina Hussein Pandu, anasema Kituo cha Afya Uzi kina hadhi ya daraja la kwanza, hivyo hakina uhaba mkubwa wa wataalamu wa afya na serikali inajitahidi kuongeza wataalamu kila inapohitajika.

"Kutokana na jiografia ya kisiwa hicho, kinahitaji kuwa na boti za kubebea wagonjwa. Serikali itakapojitosheleza katika hili haitosita kutoa huduma za uzazi katika kituo hicho maana uzazi si jambo jepesi.

"Raha ya mama anapokwenda kujifungua, arudi na mwanawe na uzazi una changamoto nyingi, lazima hivi vitu vyote vifanyiwe utaratibu ndipo shughuli za kuzalisha zitakapoanza kituoni," anasema Dk. Amina.

Anasema awali kisiwa cha Uzi hakikuwa na kituo kikubwa cha afya chenye vifaa vya kisasa na kwa sasa mama mjamzito ana uwezo wa kufanya vipimo, vikiwamo vya Utrasound, hivyo anawataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu wakati serikali inatatua changamoto zinazowakabili.

Kisera, Dk. Amina anasema kituo cha afya cha daraja la kwanza kinapaswa kutoa huduma kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri na kinapaswa kuwa watoa huduma wasiopungua 10.

Anasema Kituo cha Afya Uzi kina vifaa muhimu, vikiwamo vya dharura kwa ajili ya wajawazito kujifungulia, lakini kinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na watoa huduma.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, anasema serikali imefanya mageuzi makubwa katika sekta ya afya kwa kuboresha huduma hizo na inaendelea kuwasomesha wafanyakazi ili kuwa na wataalamu bingwa watakaotoa huduma bora kwa wananchi mijini na vijijini.

Anasema serikali pia inaendelea kuweka mazingira bora ya utoaji huduma za afya na kwamba, kwa mwaka huu wa fedha (2024/25), watumishi wapya 1,566 wataajiriwa ili kuleta ufanisi zaidi katika utoaji huduma za afya kwa wananchi.


PIER ADVOCATES

WE ARE HIRING

**Job Advertisement:** Advocates (3 Positions)
**Location:** Dar es Salaam & Mwanza
**Position Type:** Full-Time
**Experience:** 3 Years
**Application Deadline:** December 10, 2024

**Job Overview:**
Applications are invited from ambitious, energetic and performance driven individuals to fill in vacant positions mentioned above. This is an excellent opportunity for legal professionals who are keen to develop their careers in a fast-paced and challenging environment.

**Key Responsibilities:**
- Court & Tribunal Representation: Attend matters in various courts, Commission for Mediation and Arbitration (CMA), District Land and Housing Tribunal and other Tribunals.
- Pleadings & Legal Drafting: Draft pleadings, motions, and other necessary court documents for various legal proceedings.
- Registries: Assist clients with matters related to company and land registries, including filing and lodging documents, conducting search and making necessary follow-ups.
- Legal Opinions: Draft and issue well-researched legal opinions as required by clients and the Partners of the Firm.
- Partner Assistance: Provide dedicated support to specific Partners as assigned, assisting with legal research, case preparation, and other tasks as needed.
- Additional Duties: Perform other legal duties as assigned by the Firm's Partners, contributing to the overall success and growth of the Firm.

**Qualifications & Requirements:**
- LL. B degree from a recognized university;
- Admission as an Advocate of the High Court of Tanzania and Courts subordinate thereto.
- 3-5 years of post-qualification experience in a reputable law firm or legal department.
- Proven experience in civil litigation or practice in mining or corporate or business laws.
- Excellent legal drafting and research skills.
- Strong interpersonal and communication skills.
- Ability to work independently and as part of a team.
- High level of professionalism and commitment to serve clients.

**How to Apply:**
Interested candidates are invited to submit their applications, CVs, copies of academic and professional certificates to **info@pieradvocates.co.tz** by **December 10, 2024.**



PIER ADVOCATES

WE ARE HIRING

**Job Advertisement:** Office Administrator/Receptionist
**Location:** Mwanza
**Position Type:** Full-Time
**Application Deadline:** December 10, 2024

**Job Overview:**
We are looking for a detail-oriented and friendly Office Administrator/Receptionist to manage the day-to-day operations of our front office. The successful candidate will be the first point of contact for our clients and visitors, ensuring a welcoming and professional environment. In addition to receptionist's duties, the successful candidate will also support administrative tasks to ensure the smooth functioning of our office.

**Key Responsibilities:**
- Front Desk Management: Greet clients, visitors, and vendors professionally and courteously, manage the reception area, ensuring it is always tidy and presentable.
- Call Handling: Answer and direct incoming calls, take messages, and manage inquiries efficiently. Ensure that all calls are routed to the appropriate team members.
- Appointment Scheduling: Manage and coordinate appointments for lawyers and other staff members.
- Meeting Preparation: Prepare meeting rooms for client meetings, including arranging refreshments and setting up necessary equipment.
- Mail & Correspondence: Handle incoming and outgoing mail, courier services, and other correspondence.
- Administrative Support: Assist with general administrative tasks, including filing, document preparation, data entry, and maintaining office records.
- Client Assistance: Provide information and assistance to clients as needed, ensuring they have a positive experience with the firm.
- Office Coordination: Coordinate office activities and operations to secure efficiency and compliance with company policies.
- Office Supplies Management: Monitor and order office supplies, ensuring that the office is well-stocked and organized and liaise with vendors as needed.

**Qualifications & Requirements:**
- Proven experience as an Office Administrator, Receptionist, or similar role, preferably in a professional services companies/firms.
- Excellent verbal and written communication skills.
- Strong organizational and multitasking abilities.
- Proficiency in Microsoft Office Suite (Word, Excel, Outlook) and familiarity with office management software.
- Ability to maintain confidentiality, handle and keep office and clients' information secret.
- Professional appearance and demeanor.
- High School certificate or a diploma or equivalent and training in office administration.

**How to Apply:**
Interested candidates are invited to submit their applications, CVs and copies of academic certificates to **info@pieradvocates.co.tz** by December 10, 2024.



PIER ADVOCATES

WE ARE HIRING

**Job Advertisement:** Accountant
**Location:** Dar es Salaam
**Position Type:** Full-Time
**Experience:** 5 Years
**Application Deadline:** December 10, 2024

**Job Overview:**
We are looking for an experienced Accountant with a strong background in accounting and financial management. This role requires a high level of expertise in managing financial records, preparing reports, and ensuring compliance with regulatory requirements.

**Key Responsibilities:**
- Financial Reporting: Prepare accurate and timely financial statements, including income statements, balance sheets, cash flow statements, and other reports as required.
- Accounts Management: Oversee and manage the day-to-day accounting functions, including accounts payable, accounts receivable, and general ledger maintenance.
- Budgeting & Forecasting: Assist in the preparation of budgets and financial forecasts, providing insights and analysis to support business decisions.
- Tax Compliance: Ensure compliance with all tax regulations, including preparing and filing tax returns and handling tax audits when necessary.
- Internal Controls: Implement and monitor internal controls to safeguard company assets and ensure financial accuracy.
- Audit Support: Liaise with external auditors and ensure that all financial documents and records are accurate and readily available.
- Financial Analysis: Conduct regular financial analysis to identify trends, variances, and areas for improvement, and present findings to management.
- Payroll Management: Oversee payroll processing and ensure compliance with all statutory requirements.
- Regulatory Compliance: Stay updated on financial regulations and ensure the company's financial practices comply with all relevant laws and standards.

**Qualifications & Requirements:**
- A degree in Accounting, Finance, or a related field.
- CPA, ACCA, or equivalent certification is required.
- Minimum of 5 years of experience working with reputable accounting firm or other reputable company, firm or organization.
- Strong knowledge of accounting principles, financial reporting, and regulatory requirements.
- Proficiency in Tally accounting software and Microsoft Office Suite (Excel, Word, Outlook).
- Excellent analytical skills with a high level of attention to detail.
- Strong organizational and time management skills.
- Ability to work independently and as part of a team.
- High level of integrity and commitment to ethical accounting practices.
- Excellent communication and interpersonal skills.

**How to Apply:**
Interested candidates are invited to submit their applications, CVs, copies of academic and professional certificates to **info@pieradvocates.co.tz** by December 10, 2024.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matumizi mabaya ya teknolojia ni janga

**MABADILIKO** ya matumizi ya teknolojia ya mawasiliano duniani yameleta mafanikio na athari kutokana na watu wanavyoitumia teknolojia hiyo.

Mafanikio yaliyopatikana ni watu kupata fursa nyingi za kujifunza kupitia mitandao hasa inapotumika vizuri na wengine kutengeneza ajira ambazo zinawapatia vipato.

Vile vile, matumizi hayo yalisaidia kipindi ambacho dunia ilikumbwa na janga la Uviko na kusababisha wafanyakazi kuathirika na baadhi yao kupunguzwa kazi huku wengine wakilazimika kufanyakazi zao wakiwa nyumbani.

Teknolojia hiyo pia imesaidia masomo na mikutano kufanyika mitandaoni badala ya kukutana uso kwa uso na kuokoa gharama za watu kusafiri kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Hayo ndiyo matumizi mazuri ya teknolojia ambayo yanaleta tija kwa watu na nchi pia.

Hata hivyo, baadhi ya watu wanaitumia vibaya teknolojia hiyo kwa kurusha vitu vinavyozua taharuki na kuchafua watu wengine.

Teknolojia hiyo pia inatumiwa vibaya na baadhi ya watu wanaofanya uhalifu kwa kuingia kwenye akaunti za watu na kuiba fedha kimtandao na watu wengi wamelizwa kwa njia hiyo.

Kuna mambo mengi yanayotokea katika kipindi hiki huku wahalifu wakitafuta mbinu mbalimbali za kuhakikisha wanakwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Dunia kwenda na mabadiliko ya teknolojia ni kurahisisha kazi na kupunguza muda unaotumika kwa binadamu kuifanya kazi hiyo.

Pia wapo wanaotumia picha za matukio ya zamani na kuzitengeneza ili mradi kuwachafua watu na kuwaharibia wasifu wao. Teknolojia hii isitumike kuharibu badala yake itumike kujifunza mambo yenye maendeleo kwa faida yao na taifa.

Miaka ya nyuma sehemu zenye huduma muhimu kama ulipaji wa bili za umeme, maji na benki, mtu ilibidi aende kwenye ofisi hizo hali iliyokuwa ikisababisha msongamano mkubwa wa watu.

Sasa hivi hata ukiwa nje ya nchi unaweza kufanya miamala na kulipia bili zako kwa wakati.

Kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi ilikuwa inachukua muda kumtumia ndugu yake pesa, lakini kwa sasa teknolojia imerahisisha.

Lakini, teknolojia hiyo imeingiliwa na kutumika vibaya kwa baadhi ya wahalifu kwenye sekta ya fedha kwa kuwaibia watumiaji na kuwafanya waogope kuitumia.

Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA), imeeleza wazi kuwa inaendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti uhalifu mitandaoni, ikiwamo huduma za kifedha kutokana na kuongezeka mifumo mipya ya mawasiliano ya teknolojia.

Inapokuja teknolojia mpya ni muhimu ikatumika vizuri ili kunufaisha watu na kuondoa ugumu uliokuwapo mwanzo.

Kwa nchini Tanzania, wafanyabiashara, wajasiriamali wamerahisishiwa kazi kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ambapo kwa sasa wanaweza kutuma pesa nje ya nchi na kuletewa bidhaa wanazotaka badala ya kusafiri hali inayowapunguzia gharama.

Katika matumizi ya teknolojia hii pia kunahitajika uaminifu wa hali ya juu ndio maana hata TCRA ikiwa ni mdhibiti wa matumizi mabaya ya mawasiliano imekuwa ikiingilia kati kila inapoona mambo hayaendi sawa.


Kuna wanaotumia teknolojia hiyo pia kwa malengo mabaya ya kuwachafua watu wengine kwenye mitandao.

Hali hiyo imekuwa ikishamiri kwenye mitandao ya kijamii kiasi cha kuharibu hali ya hewa na wengine wanaochafuliwa huathirika kisaikolojia.

Viongozi wa juu wanapokuwa kwenye majukwaa wamekuwa wakikemea tabia hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa kama isipodhibitiwa itarudisha nyuma maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Jamii imalize uhaba wa walimu sayansi

**MWANZONI** mwa mwaka huu, Tanzania ilikuwa na uhaba wa walimu 39,610 wa masomo ya sayansi na hisabati ambao ni sawa na asilimia 55.8.

Hayo ni kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainab Katimba.

Ni taarifa anayoitoa bungeni jijini Dodoma akijibu swali la mmoja wa wabunge aliyetaka kujua nchi ina upungufu wa walimu kiasi gani wa shule za msingi na sekondari kwa masomo ya sayansi na hisabati.

Wakati kukiwa na mazingira hayo, baadhi ya wazazi na walezi wamebuni mbinu za kukabiliana na changamoto hiyo ambazo ni kuwalipa posho walimu wa kujitolea ili wazibe pengo hilo kwa muda.

Hayo yanafanyika kwenye baadhi ya shule, huku serikali ikiendelea na mchakato wa kuajiri walimu wapya kumaliza au kupunguza uhaba wa walimu katika shule za umma hasa sekondari.

Kuna maeneo wazazi na walezi wameamua kuchukua hatua za kukabiliana na tatizo hilo, kwa kuwalipa posho walimu wa kujitolea ili kusaidia kuinua kiwango cha elimu katika sekondari hizo.

Viwango vya malipo vinatofautiana wakiwamo ambao kila mmoja analipa Sh. 1,000 kwa mwezi huku wengine Shilingi 900 kwa mwezi, ili kuhakikisha watoto wao wanafundishwa masomo yote wawapo shuleni.

Juhudi za wazazi na walezi hao hazijaishia katika kulipa posho za walimu wa kujitolea tu, bali pia wanashiriki kwa hali na mali kujenga sekondari mpya zikiwamo za vijiji na kata mpya na pia vyumba vya madarasa kwa zile zenye upungufu.

Hatua hiyo inaonyesha jinsi ambavyo wanatambua kuwa shule hizo ni mali yao, wana wajibu wa kuzihudumia pale inapowezekana kwa kuboresha kiwango cha elimu kwa watoto wao.

Aidha, hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani wazazi na walezi wanashirikishwa kwa kupewa taarifa sahihi na kuhamasishwa kwa ajili ya maendeleo ya shule zao na hivyo kuwafanya wawe tayari kuzihudumia.

Shule za serikali ni za umma, ambao ni wananchi, hivyo wakati serikali ikiendelea na mchakato wa kuajiri walimu zaidi, ni muhimu umma ukabuni mbinu za kutatua changamoto zilizo ndani ya uwezo wao.

Mfano huo wa kutoa posho kwa walimu wa kujitolea ni wa kuigwa na wazazi na walezi kote nchini, kwa kuwa una mchango mkubwa kwenye maendeleo ya elimu kuliko kukaa pembeni na kudhani hawahusiki.

Ikumbukwe kuwa watoto wengi nchini, wanasoma shule za umma, ambazo zinatajwa kuwa uhaba wa walimu, hivyo ni wajibu wa umma kuzihudumia kadri inavyowezekana, ili ziwe na maendeleo mazuri.

Wazazi na wazazi wanaoishi vijijini ambako shule za huko zinadaiwa kuwa na uhaba wa walimu, ni vyema wakajiongeza kama walivyofanya wengine ambao wanawalipa walimu wa kujitolea.

Aidha, hilo linaweza kwenda sambamba na kuchangia chakula, kwa ajili ya watoto wao, na kuachana na dhana kwamba, serikali ilishazuia michango yote shuleni na kusababisha watoto wao washinde njaa.

Wataalamu wa afya wanasema, kuwalisha chakula wanafunzi shuleni kunaongeza ulinzi wa kijamii, chakula na lishe kwa wanafunzi, kuimarisha mahudhurio shuleni na kukuza mchakato wa kujifunza.

Mkakati wa kulipa posho kwa walimu wa kujitolea, ujenzi wa shule, madarasa vikienda sambamba na kutambua umuhimu wa chakula, kwa ajili ya wanafunzi shuleni, itakuwa ni hatua nzuri ya kuboresha elimu.

Wakati serikali ikiendelea kuajiri walimu, ni vyema wazazi na walezi nao wakaendelea kukabili tatizo hilo kama wanavyofanya wengine kwenye baadhi ya wilaya na mikoa.

# Wagombea waahidi kuwaondoa wanawake kwenye mikopo mwiba

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa katika Kata ya Kongowe, Halmashauri ya Kibaha Mjini wamesema vipaumbele vyao wakichaguliwa kuongoza mitaa yao ni kuwaondoa wanawake kwenye mikopo yenye riba kubwa ambayo imekuwa mwiba kwenye biashara zao.

Wametoa ahadi hiyo kwenye mikutano ya kampeni inavyoendelea kwenye maeneo yao wakisema wanawake wengi wenye mitaji midogo wanakwama kujikwamua kiuchumi kutokana na kukopa kwenye taasisi zenye riba kubwa na kuendelea kudidimia kwa kuua mitaji na kuwa na malimbikizo ya madeni ya mikopo.

Nuru Awadh, mmoja wa wagombea mtaa Miembe Saba B, ambaye alisema moja ya kipaumbele chake akipata nafasi hiyo ni kupambana na kuhamasisha wanawake kuunda vikundi waweze kunufaika na mikopo ya halmashauri.

Alisema kitendo cha baadhi ya wanawake kukosa mikopo ya halmashauri kimewasababishia kukopa kwenye taasisi za fedha zenye riba kubwa na badala ya kuinua mitaji yao, wengi wanaendelea kuwa watumwa kwa kufilisiwa na taasisi hizo.

Alisema kipaumbele chake kingine kwenye kampeni zake ni ujenzi wa zahanati na ukarabati wa barabara za mitaa ziweze kupitika muda wote.

Mboni Mkomwa, mgombea nafasi ya Mwenyekiti Mtaa wa Bamba, alisema wanawake wanataka kupata mwakilishi mwanamke atakayewasaidia kuondokana na mikopo inayoumiza.

Alisema akichaguliwa atashirikiana na wananchi na viongozi wa ngazi za juu kujenga zahanati ndani ya mtaa huo ambayo itasogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Aliahidi kuanzisha ujenzi wa shule ya msingi ambayo itawapunguzia wanafunzi kutembea umbali mrefu kuvuka barabara kuu ya Morogoro kwenda shule.

Wagombea hao wanawake ni wa nafasi ya Mwenyekiti katika mitaa sita ya Kata ya Kongowe ambao katika kampeni zao wamewasihi wananchi kuwachagua ili washirikiane na viongozi wengine kuleta maendeleo.

Akifungua kampeni katika kata hiyo, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, Silvestry Koka, alisema maendeleo yaliyopo kwenye mitaa 73 ya halmashauri mji yametokana na viongozi wa chama kimoja ambao wameshirikiana mipango na utekelezaji.

Koka alisema endapo mitaa hiyo itaendelea kuongozwa na wenyeviti wa CCM itarahisisha kukamilisha miradi iliyoanzishwa na watawashirikisha wananchi kuibua miradi inatakayowainua kiuchumi.

Diwani wa Kongowe, Hamis Shomari alisema wagombea wa CCM wote wako imara na ahadi zao wanazotoa zitatekelezwa kwa ushirikiano wa viongozi waliopo madarakani na wananchi wa maeneo husika.



Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Charles Mwamaja, akimtunuku mmoja wa wahitimu wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Shahada ya Uzamili na Uzamivu katika mahafali ya 38 yaliyofanyika chuoni hapo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wenye watoto wa ugonjwa wa kifafa waomba NHIF irejeshwe

**Na Christina Mwakangale**

WAZAZI wenye watoto wanaougua ugonjwa wa kifafa wameiomba serikali kurudisha huduma ya Bima ya Afya kupitia kifurushi cha Toto Afya Kadi kutokana na kundi hilo kukumbana na changamoto hasa kulipia huduma za matibabu.

Aidha, wameeleza kuwa tangu kusitishwa kwa utaratibu huo, baadhi ya watoto wao wameacha kutumia dawa, kuhudhuria kliniki jambo linalosababisha watoto hao kudhorota kiafya.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye kongamano la kitaifa lililoandaliwa Chama cha Wazazi Wenye Watoto wenye Kifafa Tanzania (UWAKITA), kwa kushirikiana na Idara ya Afya ya Akili Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), mwishoni mwa wiki walisema; Gharama za matibabu kwa watoto wenye kifafa ni kubwa kwa mtu mwenye kipato cha chini, jambo ambalo linatishia uhai wa watoto wao, pamoja na kuwasababishia wazazi msongo wa mawazo.

Mkazi wa Mbezi Loius Dar es Salaam, Glory Mrema, miongoni mwa kinamama ambao watoto wao wanaugua ugonjwa huo, baadhi yao wameacha kwenda hospitali kuhudhuria kliniki na kutopata dawa zaidi ya miezi tisa.

"Nashindwa kumudu gharama hizo tangu bima ya watoto ilipositishwa na serikali. Ombi langu kwa serikali, watoto wanaoishi na hali ya kifafa tuwalipie hata bima ya Toto Afya Kadi, ili wahudhurie kliniki, ombi letu kwa Rais Samia.

"Kidonge kimoja cha miligramu 500 kinauzwa Sh. 1,500 kwa bei ya rejareja. Mtoto mmoja anapaswa kumeza vidonge vinne kila siku, yaani viwili asubuhi na viwili jioni, bado dawa ya usingizi ambayo kidonge kimoja kinauzwa Sh. 500. Kwa siku moja mgonjwa wa kifafa anatumia Sh. 6,500.

"Kilio changu kwa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan atuangalie kwa jicho la pekee, watoto wanaoishi na kifafa usalama wao ni dawa na chakula. Kama mtoto mwenye hali hiyo hajanywa dawa, ndani hapakaliki, anafanya fujo nyumbani, tunashindwa kutoka katika shughuli za kutafutia kipato, tulio wengi tumeachwa na waume zetu baada ya kupata watoto hawa," alisema Glory.

Avelina Said, pia ni mzazi mwenye mtoto anayeishi na kifafa kwa sasa ana umri wa miaka 17, ambaye alianza kuugua tangu akiwa na miaka sita, alisema kilio chake kwa serikali ni kupata matibabu ya uhakika kwa mtoto wake. Alisema gharama za dawa kwa siku moja ni Sh. 6,000, hana kipato cha uhakika akitegemea kuuza karanga ambazo huzipeleka dukani kwa mtu, kutokana na kushindwa kutoka nyumbani kwenda kuziuza yeye mwenyewe kwa kuwa hana mtu wa kumwachia mtoto.

"Mume alifariki Agosti mwaka huu. Karanga natengeneza napeleka dukani kwa Mangi anaisaidie kuuza, kwa sababu nikitoka nitamwachia nani mtoto, unahitaji kumhudumia kuanzia kwenda choo, umlishe, umuogesha, shuleni aliambiwa asiende tena," alisema Avelina.

Alisema hivi sasa mtoto wake anaishi kwa kutegemea misaada na kwamba mtu ambaye atamwonea huruma humnunulia dawa za ziku tano au nusu mwezi na zinapokwisha hali ya mtoto inazidi kuwa mbaya.

"Ombi langu kuu sisi wenye watoto wanaotegemea kuishi kwa dawa, serikali ituangalie kwa jicho la kipekee tupate hiyo bima ya watoto ili watibiwe kwa uhakika," alisisitiza Avelina.

Bingwa wa Magonjwa na Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Kuganda Said, alisema bado inahitajika elimu kwa umma, kuhusu ugonjwa wa kifafa, dawa na wataalam wapo na ugonjwa unatibika.

Bingwa huyo ambaye ni Mwenyekiti wa UWAKITA, alisema chama hicho kinasisitiza elimu ya ugonjwa huo na jamii ielewe kwamba wataalamu wa kifafa wapo, vifaa vya uchunguzi vipo na ugonjwa wa kifafa unatibika, watu waache unyanyapaa kitendo ambacho ni kikubwa kwa kundi hilo.

Bingwa wa Magonjwa na Afya ya Akili wa MNH, Nuruheri Kitomary, alisema zaidi ya watu milioni 50 duniani wanaishi na kifafa, asilimia 80 wanatoka nchi zenye uchumi mdogo barani Afrika, ikiwamo Tanzania.

"Kati ya hao, watu milioni 10 wanaishi Afrika, na Tanzania inakadiriwa kuwa na watu 450,000 mpaka 500,000 wanaoishi na kifafa na ni asilimia 3.7 pekee ndiyo wapo kwenye matibabu.

"Hawa ni wale wenye usajili rasmi hospitalini, lakini kuna kundi kubwa nje ya hao ambao wamefichwa majumbani au wapo kwa waganga wa kienyeji, makanisani nakadhalika," alisema Dk. Kitomary.


Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs) na Afya ya Akili kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, alisema mkakati ni kuhakikisha vipimo na dawa phinobabitol, inapatikana katika hospitali na vituo vya afya nchini.

"Ingawa kuna dawa nyingine zaidi, lakini angalau hiyo ya msingi ambayo inasaidia kwa asilimia 70 wagonjwa wa kifafa," alisema Dk. Ubuguyu.

Dk. Ubuguyu alisema, serikali ipo mbioni kukamilisha mpango wa afya kwa wote, kila Mtanzania yakiwamo makundi tofauti atanufaika na huduma hiyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI

Simu : +255 (026) 2322703
Nukushi : +255 (026) 2322704
Baruapepe: km@uchukuzi.go.tz
Tovuti: https://www.uchukuzi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba, 1 Mtaa wa Ujenzi,
S. L. P 638,
40470 DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA

### TANZANIA KUWA MWENYEJI WA MKUTANO MKUU WA SABA (7) WA JUMUIYA YA MAMLAKA ZA USIMAMIZI WA USAFIRI MAJINI AFRIKA

***Novemba 25, 2024 – Dodoma.***

Wizara ya Uchukuzi inautaarifu umma na wadau wa sekta ya usafiri majini kuwa Tanzania kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeteuliwa kuwa nchi mwenyeji wa Mkutano wa Saba (7) wa Kimataifa wa Jumuiya ya Mamlaka za Usimamizi wa Usafiri Majini Barani Afrika, utakaofanyika kuanzia tarehe 29 Novemba hadi 01 Desemba, 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Lengo la mkutano huu ni kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya udhibiti na usimamizi wa usalama wa usafiri majini barani Afrika huku kipaumbele kikiwa ni mustakabali wa usafiri wa majini na kuongeza ushirikano baina ya nchi wanachama.

Kauli mbiu ya mkutano huo ni **"Kuimarisha mustakabali wa sekta ya usafiri majini barani Afrika: Ushirikiano katika Teknolojia na Ubunifu ili kupunguza hewa ukaa, kuimarisha usalama, na mazingira ya sekta ya usafiri majini kwa mustakabali endelevu".**

Mkutano huo utatumika kama jukwaa muhimu katika kuwezesha wadau kushiriki katika majadiliano yanayogusa masuala ya teknolojia na ubunifu yenye kulenga katika kuimarisha usalama na mazingira ya usafiri majini, pia, watapata fursa ya kuingia makubaliano ya kibiashara pamoja na kuanzisha mitandao na ushirikiano katika uendeshaji masuala mbalimbali yanayohusiana na fursa za uchumi wa buluu.

Mkutano huu wa kihistoria utafunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na utahudhuriwa na Katibu Mkuu wa Shirika la Bahari Duniani (IMO), Bw. Antonio Dominguez pamoja na wataalam wa usafiri majini, viongozi wa mamlaka za udhibiti wa usafiri kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, zipatazo 50 ambazo zina bahari, maziwa na mito na wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya Kimataifa.

Ushiriki wa Bw. Dominguez ni heshima kubwa kwa Tanzania hasa kipindi hiki tunapotekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu, ambapo kama nchi tumebainisha masuala ambayo Serikali kwa kushirikiana na wadau, kuhakikisha nchi inanufaika na fursa zitokanazo na rasilimali za Uchumi wa Buluu ili kukuza uchumi wa Taifa kwa maendeleo endelevu.

Aidha, Tanzania itaendelea kutangaza fursa za kiuchumi zilizopo katika sekta ya usafiri kwa njia ya Maji zinazohusiana na utumiaji wa rasilimali za bahari na maziwa pamoja uchukuzi ili kukuza uchumi wa buluu, kufanya tafiti na kuwekeza katika uvunaji wa rasilimali bahari na maziwa zitakazosaidia kuongeza uwezo wa Serikali kuwahudumia wananchi na kuwaleta maendeleo endelevu.

Tunatoa wito kwa wadau wote wa sekta ya usafiri majini, wakiwemo wasafirishaji, wamiliki wa vyombo vya usafirishaji majini, wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, viongozi wa Serikali kujitokeza kwa wingi kuhudhuria mkutano huu muhimu ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha usafiri wa majini hapa nchini Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

Katika Mkutano huo pia kutakuwa na maonyesho na utoaji elimu kwa umma na washiriki watakao shiriki katika mkutano huo, hivyo tunawakaribisha wananchi wote.

**Imetolewa na:**

**Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb)**
**WAZIRI WA UCHUKUZI**

# Wafa baada ya nyumba kusombwa na maji

**Na Waandishi Wetu,** TARIME

WATU tisa wa familia mbili za Ochieng Moses na Elias Ngare katika mtaa wa Bugosi, kata ya Nyamisangura, Halmashauri ya Tarime Mji, mkoani Mara wamefariki dunia huku wawili wakinusurika baada ya nyumba kusombwa na maji usiku wakiwa wamelala.

Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Tarime, Elias Kabinga alisema walipokea taarifa usiku juu ya watu kusombwa na maji katika mtaa huo.

Alisema kuwa walifika na kufanikiwa kuwaokoa watu wawili - mwanamke na mwanamume na baadaye kuopoa miili ya watu saba, sita ikiwa ni ya wanawake.

"Miili hiyo imeopolewa maeneo ya Utegi, wilayani Rorya zaidi ya Km 30 kutoka eneo la tukio maana nyumba hiyo ilikuwa imejengwa kando ya mto wenye mkondo wa maji yanayoelekea katika eneo hilo," alisema Kabinga.

Alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanaendelea kutafuta miili ya watoto wawili wenye umri wa mwaka mmoja na nusu na mwingine mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi mitatu ambao bado hawajapatikana.

Aliwataka wananchi waliojenga karibu na mito au mabondeni, wahame kwa kuwa mvua inaendelea kunyesha na inaweza kuhatarisha maisha yao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya Tarime, Dk. Yonam Charles, alisema walipokea miili ya watu watano iliyoopolewa kwa kusombwa na maji pamoja na majeruhi wawili walionusurika ambao ni Ochieng Moses na Wilfrida Isaya. Wamelazwa hospitalini huko wakiendelea kupatiwa huduma tangu walipofikishwa usiku wa kuamkia jana.

Akisimulia tukio hilo, Diwani wa Kata hiyo, Thobias

Ghati ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime Mji, alisema kuwa usiku wa kuamkia jana, ilinyesha mvua kubwa na kusababisha madhara hayo kwa familia hiyo iliyokuwa imejenga kando ya Mto Mori.

Alisema tukio hilo lilizikumba familia mbili; moja ikiwa na watu 10 (wamenusurika watu tisa) huku nyingine ikiwa na watu tisa (mmoja tu aliyenusurika), nyumba zao walimokuwa wanaishi zimesombwa na maji.

Akiwa katika eneo la tukio, Ofisa Tawala wa Wilaya ya Tarime, Sauli Mwaisenye alisema walipopata taarifa juu ya wananchi hao kusombwa na maji, walifika eneo la tukio na kukuta miili ya watu saba imeopolewa na watu wengine wawili wameokolewa na jitihada za kuwatafuta wengine zinaendelea huku akiwataka wanafamilia kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, akiwamo Rose John, waliomba halmashauri kuwaondosha watu waliojenga kando ya mito ili kudhibiti madhara ya namna hiyo ambayo yamekuwa yanatokea kila inyeshapo mvua kubwa.

***Imeandaliwa na Samson Chacha na Timoth Itembe.**

# TCRA, ANADEN ya Comoro kuingia makubaliano

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini inatarajia kuingia makubaliano ya ushirikiano kwenye masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Wakala wa Maendeleo ya Huduma za Mtandao nchini Comoro (ANADEN).

Hayo yamesemwa mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kubadilishana uzoefu iliyofanywa na Mkurugenzi wa wakala hiyo kwenye Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano.

Akiambatana na ujumbe kutoka ANADEN, Balozi wa Shirikisho la Visiwa vya Comoro nchini, Said Yakub pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Huduma za Mtandao, Said Moinuo Ahamada, walisema ni heshima kupata fursa ya kujifunza na kuona namna Tanzania kupitia Mamlaka ya Mawasiliano ilivyopiga hatua kubwa kwenye sekta ya mawasiliano.

Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Mhandisi Felician Mwesigwa akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Jabir Bakari, aliwapongeza kwa kuchagua Tanzania kwa ajili ya kupata uzoefu wa masuala ya TEHAMA.

Awali, akiwasilisha kazi na majukumu ya TCRA alisema Tanzania inajivunia kwa hatua kubwa iliyofikiwa kwenye maendeleo ya TEHAMA kwa kuwa na kituo kikuu cha kitaifa cha taarifa.

Mkurugenzi wa ANADEN, Said Moinuo Ahamada alisema dhumuni la ziara hiyo ni kujifunza kwa ajili ya kuona Comoro inavyoweza kupata wataalamu watakaowezesha kuanzishwa kwa mifumo ya kuhudumia serikali.

Mifumo hiyo ni Wakala wa Serikali Mtandao, Kikoa cha Kitaifa (Domain Names) na kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Taarifa, vyote vitachangiza ukuaji wa matumizi ya mtandao kwenye shughuli za serikali na binafsi.

Aidha, alisema Comoro inatarajia kupokea msaada wa fedha toka Benki ya Maendeleo Afrika (ADB) ambazo zitatumika kwenye maendeleo ya TEHAMA kupitia ANADEM.

"Tunaamini kupitia fedha hizi tutafanya maboresho kwenye mifumo yetu ya mtandao kama vile kuongeza uwezo kwa wataalamu wetu na kuboresha uwezo wa mifumo kuwasiliana," alisema.

Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Yakubu alisema matumaini yake ni kuwa Hati za Ushirikiano baina ya TCRA na ANADEM ni kubadilishana wataalamu na uwezo kuiwezesha nchi hiyo kupiga hatua kwenye eneo la TEHAMA.



## Mapango ya Amboni kuwekwa taa, marekebisho lango kuu

**Na Godfrey Mushi,** TANGA

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa mapango ya Amboni yaliyoko nje kidogo ya Jiji la Tanga.

Maboresho hayo ni pamoja na kuweka taa ndani ya mapango, ujenzi wa lango kuu, kuimarisha mifumo ya malipo na kuongeza ulinzi wa eneo hilo, ili kuongeza chachu katika utalii wa malikale.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Elirehema Doriye, mradi huo unalenga kuhakikisha inalinda, inahifadhi na inaimarisha vivutio vya malikale inavyoyovisimamia.

Dk. Doriye alikuwa akizungumza na watumishi mbalimbali, baada ya kutembelea mapango hayo juzi.

Alisema mapango ya Amboni ni moja ya vituo vya malikale, ambayo NCAA imedhamiria kuhifadhi, kuendeleza, kuboresha na kuyatangaza zaidi ili kuongeza idadi ya wageni wanaotembelea mapango hayo.

Dk. Doriye ameeleza zaidi kuwa: "Kwa sasa NCAA, inaendelea kutanua wigo wa mazao mapya ya utalii ili kuongeza vyanzo vya mapato na kuongeza mtawanyiko wa wageni hasa katika vituo vya malikale.

"Tunamshukuru Rais, Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kutuongoza vizuri katika kusimamia sera na mipango yetu ya kuongeza vyanzo vya utalii, na mamlaka haitowaangusha viongozi wetu hao," alisema Dk. Doriye.

Mapango ya Amboni yamebeba historia kubwa ya harakati za kudai uhuru ambapo inaelezwa kuwa baadhi ya wapinga ukoloni waliyatumia katika harakati za kudai uhuru wa nchi.

Vilevile, mapango hayo ni moja ya vituo vya malikale vinavyosimamiwa na NCAA.

Vituo vingine ni eneo la Engaruka lililoko Monduli, majabali ya Mumba yaliyopo Karatu, kimondo cha Mbozi kilichopo Mkoa wa Songwe pamoja na Makumbusho ya Bonde la Olduvai lililopo Ngorongoro.

# Jussa awapa ujumbe polisi kuelekea Uchaguzi S/mitaa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo Zanzibar, Ismail Jussa, amevishauri vyombo vya usalama kuacha kutumia mabavu katika uchaguzi, bali watekeleze majukumu yao ya kulinda amani.

Jussa, alieleza hayo jana alipokuwa mkoani Tanga kushiriki kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kupitia chama hicho katika Mkoa wa Tanga ambapo aliwataka kutekeleza jukumu lao la msingi la kulinda raia na mali zao.

Aidha, aliwataka kuwaacha wananchi waweze kushiriki kwa amani katika kampeni hadi siku wanapokwenda kupiga kura kuacha tabia ya kuwatisha kwani hii nchi ni ya demokrasia.

"Niwaombe polisi acheni kuwafanyia wananchi vitisho kwani najua mtasumbua sana siku za mwisho za kampeni na siku ya uchaguzi.

...Ili tuonekane wapinzani tunavurugu safari hii hatutatii, timizeni majukumu yetu uchaguzi tuachieni sisi wananchi tukaamua kwa haki na amani," alisema Jussa.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wa Tanga kutokufanya makosa katika uchaguzi huu kwa kuchangua viongozi wa serikali za mitaa wanatokana na chama hicho ambacho tayari kina sera ya uchaguzi huo.

"ACT ndio chama pekee ambacho safari hii kimekuja na Sera ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ambayo imeainisha vipaumbele vyake kwa ajili ya maendeleo ya wananchi," alisema Jussa.

Naye Mjumbe wa Kamati Kuu Taifa ya ACT Wazalendo, Rehema Mohamed, alisema kuwa chama hicho, kimeweka mawakili watatu ambao watashughulika na mashauri ya uchaguzi.

Alisema: "Niwahakikishie wananchi wa Tanga kuwa awamu hii hatutakubali kuonewa na kama tukishindwa kupata haki yetu kwa wananchi tunakwenda kuidai mahakama."



Waandishi wa habari mkoani Manyara kwa kushirikiana na muungano wa vilabu vya waandishi habari Tanzania (UTPC) wakiwa kwenye maandamano ya amani katika uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Wanawake jamii za asili wakutana kujadili athari mabadiliko tabianchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAKUNDI ya wanawake kutoka makabila na jamii za asili nchini, wamekutana jijini Arusha, kujadili changamoto zinazowakabili kwa sasa, ikiwamo athari za mabadiliko ya tabianchi.

Wanawake hao kutoka jamii za Wahadzabe, Wamasai, Wabarbaigi, Wadatoga na Waakei, wameeleza kuwa mabadiliko ya tabianchi yameleta ukame katika maeneo mengi ya jamii hizo na hivyo kuathiri maisha yao.

Jana, wakati anafungua kongamano la siku mbili la wanawake wa jamii za asili, Mkurugenzi wa Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Jamii (CORDS), Lilian Looloitai, alisema wanawake wa jamii za asili wanakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, yaliyopelekea kuwepo na vikwazo vya kiuchumi na kijamii.

Alisema mabadiliko ya tabianchi, yameathiri maisha ya kila siku kwa wanawake wafugaji na waokota matunda, hivyo ni muhimu kwa wanawake hao kuwa na mtandao wa pamoja utakaosaidia kufikia malengo ya uongozi na maendeleo ya uchumi kwa jamii hizo.

Kadhalika, alisema mtandao huo utatoa fursa kwa wanawake wa asili kuwa na ujasiri wa kugombea nafasi za uongozi pamoja na mawasiliano ya jamii zote.

Mjumbe wa Bodi ya CORDs, Adam Ole Mwarabu, akizungumza katika kongamano hilo aliwataka wanawake wa jamii ya asili kuendelea kutunza mila na tamaduni zao.

Ole Mwarabu, alisema licha ya maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia bado kuna haja ya kuendelezwa mila na desturi za jamii za asili.

Aidha, alisema jamii za asili zinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwepo masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, lakini umoja na mshikamano utasaidia kutatua changamoto hizo.


Regina Gapchojiga kutoka jamii za Wabarbaigi, alisema kuwa wanawake wa jamii hiyo wameathiriwa mno na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mifugo kufa na hivyo kulazimika kuhamisha iliyopo kwenda kutafuta malisho nje ya Wilaya ya Hanang' na hivyo kuathiri uchumi wa kaya zao.

Janeth Kamunyu kutoka Shirika la Kinyok Indigenous Pastoralists Women Organization (KIPWO), lililoko Mvomero, mkoani Morogoro, alisema kongamano hilo litawasaidia kuwa na sauti ya pamoja kujua changamoto zinazowakabili wanawake wa asili nchini.

Ofisa Jinsia kutoka Shirika la CORDS, Martha Katau, alisema kongamano hilo ni muhimu, kwani limewakutanisha wanawake wa jamii za asili nchini na kujadili utatuzi wa changamoto za jamii za asili nchini.

Anna Matinda, Ofisa Utawala CORDS, alisema wanaimani kongamano hilo litasaidia kuwaunganisha wanawake na kuwa na sauti moja katika utetezi wa jamii za asili.

Kongamano hilo la kwanza kwa wanawake wa jamii za asili linatarajiwa kufanikisha kuanzishwa kwa mtandao wa wanawake wa jamii za asili nchini.



# Ukata chanzo TLS kujiweka kando Uchaguzi S/mitaa

**Na Vitus Audax**, MWANZA

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimevunja ukimya juu ya kutokuingilia moja kwa moja malalamiko ya vyama vya siasa kuhusu ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi alisema hayo wakati wa mahojiano na Nipashe jijini Mwanza kuhusu tathmini ya mchakato mzima wa uchaguzi.

Alisema kuwa kwa sasa hali ya mfuko wa chama hicho siyo mzuri na wamekosa mdhamini ili kuweka mawakili wa kuendesha kesi hizo zenye maslahi kwa umma na kuwa suala hilo siyo la kutolea matamko pekee bali kuchukua hatua.

Mwabukusi alisema mchakato huo unahitaji nguvu kazi pamoja na fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli mbalimbali ikiwamo kuendesha mashauri, lakini kwa sasa chama hicho hakina bajeti ya kuweza kudhibiti uvunjifu wa sheria na kuwa wanajipanga ili kutekeleza hayo katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

"TLS tunayo nguvu kazi kubwa na lakini tatizo kwa sasa lipo kwenye bajeti ya kifedha. Wakati naingia kwenye nafasi hii niliweka jitihada kubwa katika kuhakikisha TLS inadhibiti ukiukwaji wa sheria katika uchaguzi lakini siwezi kulaumiwa kwa lolote na yeyote kuwa sikumshirikisha katika kupata uwezeshaji kwenye hili."

"Mpaka sasa tumewafuata wengi lakini hakuna aliyekuwa tayari kutusaidia kwani wapo waliosema ni ghafla mno, wengine walisema haipo kwenye bajeti yao, wengine hawana hiyo programu huku wengine wakisema ni haraka sana kwa hiyo hatukuliweka kwenye programu zetu mwaka huu bali tutaliweka mwakani kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025," alisema Mwabukusi.

Kuhusu tathmini ya chama hicho juu ya mwenendo mzima wa uchaguzi, Mwabukusi alisema, kwa asilimia kubwa wamebaini kukiukwa kwa sheria kuanzia uandikishaji mpaka mchakato wa uteuzi wa wagombea, akidai wasimamizi wamekuwa wakikiuka hadi maelekezo ya mamlaka waziwazi.

Aidha, alitaja uvunjifu katika uchaguzi huo kuwa ni pamoja na kuandikisha watu wasiokuwa na vigezo ikiwamo wanafunzi wenye umri chini ya miaka 18 na kuwa licha ya kelele nyingi hakuna kilichofanyika, vilevile alitaja kuenguliwa kwa wagombea kwa sababu zisizo za kikanuni.

Aliwataka wasimamizi waliopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi kuhakikisha wanatenda haki na siyo kufuata misukumo binafsi.



Veronica Mlimadago Mkazi wa Kijiji cha Kiloleli, wilayani Kishapu, akichota maji kwenye bwawa la Kiloleli juzi, kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya nyumbani ikiwamo kunywa, wamedai maji hayo siyo safi na salama kutokana na kijiji hicho kutokuwa na huduma ya majisafi na salama. **PICHA: MARCO MADUHU**

## CHADEMA yang'oa makada 12 wa CCM Tarime

**Na Samson Chacha**, TARIME

WAKATI shughuli za kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zikitamatishwa leo, makada 12 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Tarime mkoani Mara wamejiunga na CHADEMA

Makada hao ni pamoja na aliyekuwa Mwenyeviti wa Kijiji cha Pemba, Christopher Wantora, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mlimani, Werema Nyaisaro, Katibu wa Tawi la CCM Kitongoji cha Sokoni Kata ya Sirari, Sererya Nyaragita pamoja na wanachama wengine 10.

Akiwapokea wanachama hao wapya wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika mwishoni mwa wiki katika Mji wa Sirari, Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (BAWACHA), Mkoa wa Mara, Veronika Sando, alisema hatua hiyo ni ishara ya uimara wa sera za chama hicho katika kuwatumikia Watanzania.

Aidha, aliwataka kinamama, vijana na wazee kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura ili kuchagua wagombea wa chama hicho.

Mwenyekiti CHADEMA Wilaya, Mwita Isasi aliwapongeza kwa kujiunga chama hicho alichokitaja kuwa ni kimbilio la wanyonge, kutetea haki za wananchi, kupambana na vitendo vya rushwa na unyanyasaji kwa kuwanyima wananchi haki zao.

Aliyekuwa Mwenyeviti wa Kijiji cha Pemba, Christopher Wantora, alisema yeye pamoja na wenzake wameamua kuhama katika chama hicho kutokana na alichokiita kuwa ni unyanyasaji.

**Aidha, aliwataka kinamama, vijana na wazee kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura ili kuchagua wagombea wa chama hicho.**

# Wananchi watakiwa kutouchukulia poa Uchaguzi S/mitaa

**Na Waandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Zanzibar, Salumu Mwalimu, amewataka wananchi wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kutokuchukulia poa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kwani ndiyo sehemu ya kuandaa na kupata viongozi bora wa ngazi za kata, majimbo na taifa.

Mwalimu aliyabainisha haya juzi wakati akiwanadi wagombea wa chama hicho katika nafasi ya Mwenyekiti wa Mtaa, Kijiji, Vitongoji na wajumbe katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Kagongwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Pamoja na mambo mengine, Mwalimu aliwasisitiza wananchi hao kwamba endapo watapata ridhaa watatokomeza vitendo vya rushwa.

Alisema wananchi hususani vijana wamekuwa na tabia ya kuchukulia poa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kutokujitokeza siku ya tarehe ya uchaguzi kuchagua viongozi wanaowataka.

Alisema wananchi wengi wanachojari ni kupata kitambulisho cha mpigakura na kufanya mambo yao, huku wakipoteza haki yao ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa.


Mwalimu alisema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndiyo uchaguzi mkubwa kulinganisha na Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais kwa sababu kila kitu kinachotakiwa kufanyika huwa kinaanzia serikali za mitaa.

"Hata ukitaka kupata hati ya kusafiria, kitambulisho cha taifa, akaunti za benki lazima upate mhuri wa mwenyekiti wa mtaa wako hakikisheni ifikapo Novemba 27 tujitokeze kwa wingi kwenye vituo vya kupigia kura na kuchagua viongozi tunaowahitaji," alisema Mwalimu.

Katika hatua nyingine Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko akiwa wilayani Chato aliwataka wananchi wilayani humo kutokufanya makosa katika uchaguzi huo kwa kuwapa nafasi watu wasioweza kuwahudumia ipasavyo na kutatua matatizo yao.

Alisema: "Ili miradi inayotekelezwa iwe na uendelevu na ile iliyotekelezwa iendelee kuwanufaisha ni vyema kuchagua viongozi wenye nia ya kuendelea kuwaletea maendeleo, huku akivitaka vyama vya upinzani kushindana kwa hoja na siyo matusi ili kuhakikisha vinakuwa nyenzo ya kuunganisha na siyo kuwagawa Watanzania".

***Imeandaliwa na Shaban Njia (Kahama), Vitus Audax (Mwanza)***



Ukurasa 12

**Usichekelee kipara cha ghafla ni tatizo mwilini**



Ukurasa 13

Binti anapotosa mipango ya kuozwa utotoni kisa mahari ya ng'ombe saba na Sh. 200,000



Ukurasa 14

**Mtaalamu anaposisitiza umuhimu mbolea shambani, kuua viuatilifu kwenye udongo**

Nipashe

# TESA

Jumanne Novemba 26, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# TANCDA inapobaini kupenda kuketi zaidi kunasababisha kufa haraka

UTAFITI unaofanyika hivi karibuni umebaini kuwa kwa kila saa unayoketi iwe kuangalia runinga au kupiga gumzo kijiweni unapunguza uhai wako kwa dakika 22.

Sasa kazi kwako angalia unatumia saa ngapi kupiga umbea, kushinda kijiweni kwenye biashara za wenzako, au kuangalia runinga ukiwa umekaa na ufanye mahesabu dakika ulizopoteza kwenye miaka ya uhai wako.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukizwa Tanzania (TANCDA), licha ya kwamba utafiti huo haukufanyika Tanzania, wanasisitiza kuwa kuketi kwa zaidi ya saa moja mfululizo kuna athiri nyingi.

Mosi, kunaathiri uwezo wa mwili kuchakata sukari, huleta shinikizo la damu na mwili kutumia mafuta hivyo kuongeza uwezekano wa kuugua moyo, figo, kisukari na saratani.

Shirikisho linasema vile vile kuketi huko huongeza uwezekano wa mwili kushindwa kunyooka ipasavyo na kusababisha maumivu ya mgongo na hata kukunjika uzeeni.

Taarifa hizo zipo kwenye machapisho yao kuhusu magonjwa yasiyoambukiza pamoja na elimu ya utaalamu waliyotoa kwa wafanyakazi wa IPP Media, walipowatembelea kwa ushauri na vipimo vya maradhi ya kisukari.

Aidha, wataalamu wanasema kuketi muda mrefu kunaathiri afya ya akili na kushauri kuwa ni lazima kutembea, kujinyoosha kwa dakika mbili kila baada ya kuketi kwa saa moja.



Vijana waepuke kukaa bila kazi vijiweni ili kulinda afya zao. **PICHA: MTANDAO**

Lakini pia wanashauri kuacha mtindo wa ubwete na kuushughulisha mwili, iwe kusimama, kutembea, kufanyakazi badala ya kujipumzisha kwenye viti.

Kwa mfano, umeanza kazi saa 3:00 asubuhi ikifika saa 4: 00 kama ulikuwa umekaa kwenye kiti ukihudumia wagonjwa, kufundisha darasani au kuchapa kazi kwenye kompyuta simama na tembea kuifanyisha misuli kazi.

Tembea umfuate mwenzako kueleza haja yako, achana kupiga simu au kutuma SMS, ukipigiwa simu au kupiga ongea ukiwa umesimama siyo kukaa muda wote.

"Pia punguza muda wa kuketi mfululizo kuangalia runinga, au kompyuta, kusogoa, badala yake ongeza muda wa kufanya mazoezi hasa kusimama wima badala ya kuketi."

## NDIKO KUJIMALIZA

TANCDA inakumbusha kuwa mwanadamu anapozaliwa misuli yake haijui kazi, kwani kwa miezi tisa ililala tumboni kwa mama bila shughuli.

Baada ya miezi sita tangu kuzaliwa, mtoto anaanza kukaa na zaidi ya mwaka mzima anahitajika kujifunza kutembea na kukimbia.

"Tunahitaji uzoefu kuendelea kutumia misuli yetu karibu kila siku ili kudumisha uzoefu huu. Bila shughuli misuli inasahau jinsi ya kutumia sukari na kutojishughulisha, ikumbukwe misuli isiposhughulishwa inasahau kutumia sukari na kutoshughulisha misuli ni moja ya visababishi vya kisukari, saratani, magonjwa ya moyo, na mishipa ya fahamu."

Shirika la Afya Duniani (WHO), linakadiria kuwa kutokuushughulisha mwili kunachangia asilimia sita ya vifo vyote duniani, asilimia 17 ya magonjwa ya moyo, na kisukari asilimia 12 ya kuanguka kwa wazee na asilimia 10 ya saratani ya matiti na utumbo mpana.

Wataalamu wa magonjwa yasiyoambukiza wanaonya kuwa bila kuushughulisha mwili hauwezi kufanyakazi kakamilifu na ushauri wao ni kufanya mazoezi kama kutembea, kuendesha baiskeli, kushiriki michezo na burudani.

Kufanya mazoezi ni lazima ili misuli iwe imara angalau nusu saa kila siku. Zipo njia tano za kufanya mazoezi kila siku kwa mfano, ukiwa kazini, shuleni au nyumbani, kusafiri, kushiriki michezo, kucheza muziki na kazi za kijamii.

Inasisitizwa kuwa tendo lolote linalohusisha misuli na kuongeza mapigo ya moyo au kasi ya kupumua au mwili kutoka jasho, liwe ni kazi, kusafiri, michezo au burudani.

Kadhalika zinahitajika shughuli za kulainisha viungo, kuimarisha misuli na kutuwezesha kufanyakazi bila kuchoka haraka. Tunahitaji tuweze kukimbia, kuruka juu, wepesi kukata kona na kukwepa vitu bila kuanguka na pia kujikunja kama mtu atahitajika kupita sehemu nyembamba au kuketi chini sakafuni.

## KULALA NI MUHIMU

TANCDA inashauri kulala kwa muda mahususi kulingana na umri, mathalani watoto wa miaka sita hadi 13 wanapaswa kulala saa tisa mpaka 11, wakati vijana wa miaka 14 hadi 17 watumie saa nane hadi 10 kulala.

Inashauri pia kwamba wenye miaka 14 hadi 64 walale saa saba mpaka tisa kila siku wakati wazee kuanzia miaka 65 walale kwa saa saba hadi nane.

INAENDELEA UK.12

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Usichekelelee kipara cha ghafla ni tatizo mwilini

KUPUKUTIKA nywele si jambo jema, wala la kupuuza. Usifurahie kipara kuna tatizo.

Makala ya BBC Swahili inasema chakula unachokula ni muhimu katika kuufanya mwili kuwa na afya njema na kiakili pia, wakati hayo yakitokea mlo huo huathiri kila kitu kuanzia nywele, mifupa na ngozi pia.

Kunyonyoka nywele sio jambo dogo, kadhalika kuona zinapotea isivyo kawaida ni ishara ya kwanza kwamba kuna tatizo na mtu hapaswi kupuuza.

Kupururuka nywele kunaweza kusababishwa na mambo kadhaa kama msongo wa mawazo, pengine kuna uhusiano na vinasaba, mabadiliko ya homoni au matumizi ya dawa au tiba ya maradhi fulani.



Upara na nywele za mvi ni ishara za magonjwa ya moyo. **PICHA/MAKALA: BBC**

**VYAKULA VINAVYOFAA**

Baadhi ya vyakula vyenye protini nyingi kama mayai na dengu, vitamini B kama mayai, maparachichi, madini ya chuma na zinki hasa nyama na njegere ni muhimu kuwa na nywele zenye afya.

Aidha, ikumbukwe kuwa mpangilio mbaya wa mlo kuwa na uzito mdogo na kula kupita kiasi, yanahusishwa sana na kunyonyoka nywele. Huenda isijulikane hasa ni mambo gani maalum ya lishe husababisha kunyonyoka nywele lakini ukweli ni kwamba chakula ni kila kitu.

Lakini, kwa mfano, vyakula vyenye sukari nyingi na mafuta kwa wingi si tu husababisha ugonjwa wa moyo, lakini pia matatizo na kuvimba seli.

Kwa haya miili hupokea mabadiliko na kukumbwa na kadhia ikiwamo kunyonyoka kwa nywele.

Bado haijafahamika rasmi ni chakula gani hasa kinachosababisha kunyonyoka nywele, lakini kwa mfano milo iliyojaa mafuta na sukari tele inatajwa kuudhoofisha mwili ni wazi hata nywele haziwezi kubaki salama.

Vyakula vilivyo na lishe inayozuia tatizo hili kama samaki na mafuta ya mbegu vinapaswa kupewa kipaumbele, baadhi ya mitazamo hushauri kuepuka vyakula vinavyosababisha kiungulia kwani vinaweza kutishia afya ya nywele, tafiti nyingi zinaunga mkono hilo.

Kwa mfano, wengine husema kwamba kufuata mlo wenye matunda mengi, mboga, nafaka, njugu, mbegu na mafuta asilia, ambayo yana sifa nyingi za kuzuia kiungulia, inaweza kusaidia kudumisha afya ya nywele.

**VISABABISHI**

Sababu nyingine kuu ya kupoteza nywele ni msongo wa mawazo, ambao huongeza kiwango cha homoni ya 'cortisol' katika mwili. Ikiwa homoni hii itatolewa kwa wingi sana au kidogo, kutakuwa na matatizo.

Msongo wa mawazo umekuwa wa kawaida katika maisha ya kila siku. Ikiwa hali hizi za msongo zinaendelea kwa muda mrefu, tatizo la kunyonyoka kwa nywele huanza. Homoni ya Cortisol inayozalishwa na tezi ya 'adrenal' inahusiana na kupoteza nywele.

Msongo unapopungua, viwango vya homoni hii katika mwili vitarudi kwa kawaida.

Lakini swali linabaki, inawezekana kudhibiti uzalishaji wa homoni hii kwa kutumia chakula? Jibu ni inawezekana.

Homoni ya Cortisol inaweza kuzuiwa kwa kujumuisha maparachichi, samaki wenye mafuta mengi kama sangara, mbegu, vyakula vilivyo na omega-3 fatty acids, vitamini na madini mbalimbali.

**VYAKULA VICHACHU**

Vyakula vilivyochachushwa vimethibitishwa kuwa vyema katika kudhibiti upotevu wa nywele.

Hapa ndipo jukumu la "gut microbiota" au matrilioni ya bakteria waishio ndani ya utumbo ambao ni muhimu.

Microbiota ni vijidudu ambavyo vinaishi katika mfumo wa kusaga chakula na mara nyingi ni muhimu mno, wanahusika katika afya na magonjwa huingiliana na virutubisho vinavyotumiwa, katika miili ambavyo hutofautiana kulingana na chakula watu wanachokula.

Mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na urutubishaji wa lishe katika miili hutegemea idadi ya microbiota, idadi yao, ishara mbalimbali za kemikali na kimmeng'enyo wa chakula hutolewa katika mwili, husaidia pia kukabiliana na msongo wa mawazo.

Ikiwa lishe ni tofauti, ndivyo ilivyo hata bakteria kwenye utumbo. Kwa hivyo kutumia vitu kama mtindi pamoja na vyakula vingine vilivyochachushwa vinaweza kusaidia kuimarisha afya ya nywele.

Kwa kufuata maelekezo hayo nywele zitakuwa na afya, kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha San Jorge Sayansi ya Afya PDI Kitivo Pilar Argento Arizona.

## TANCDA inapobaini kupenda kuketi zaidi kunasababisha kufa haraka

**INATOKA UK.11**

"Jizoeshe kulala saa ile ile kila siku. Mfano kama ni saa 4:00 usiku fanya hivyo siku zote. Amka muda ule nyakati za asubuhi kama ni saa 11:30 hata kama ni sikukuu au likizo ama mwisho wa juma." Inasema TANCDA.

Wataalamu hao wanakumbusha kuwa kuzingatia muda wa kulala kunajenga vichocheo au homoni za kukabiliana na msongo wa mawazo (sonona) na kuimarisha afya ya mwili.

Aidha, kunaondoa uwezekano wa kupata maradhi ya kisukari, shinikizo la damu, unene kupindukia, figo na sonona.

Ufanisi na usalama kazini na umakini darasani unapungua iwapo mtu hatalala vya kutosha.

**ANGALIZO**

TANCDA inawashauri Watanzania kuacha kutumia vitanda kwa shughuli zisizohusiana na kulala na eneo hilo liwe ni sehemu ya kupumzisha mwili.

"Usikitumie kitanda kuangalia runinga, kufanyakazi kwenye kompyuta, kuangalia simu, kuandika, kusoma magazeti na vitabu. Ni vyema ukaizoesha akili yako kuwa kitanda ni sehemu ya usingizi." Inasema TANCDA.

Iwapo usingizi hauji, ondoka na kufanya kazi kitu kitakachofanya upumzike badala ya kuwaza changamoto zako, mfano kusoma vitabu vya hadithi, maandiko matakatifu lakini pia kufanya mazoezi mepesi.

Wanashauri urudi kitandani mara moja unapoona usingizi unaanza kuja.

**KUVUTIA USINGIZI**

TANCDA inashauri ili kuwa na mazingira ya kulala kwa furaha na utulivu punguza mwanga chumbani, ondoa kompyuta na runinga, pia chumba kiwe na hewa ya kutosha, kuwe na ubaridi na kuepuka kuangalia saa mara kwa mara kwani vinaondoa utulivu na kusababisha ushindwe kulala.

Wataalamu hawa wanashauri kuepuka kutumia muda mwingi kulala mchana au kusinzia kwenye kiti, daladala na kwingineko. Hii hupunguza muda wa kulala nyakati za usiku.

**KUMBUKA MAZOEZI**

Kufanyakazi au kuushughulisha mwili ni chanzo cha kubaki imara na kuonekana kijana kwa muda mrefu zaidi.

Kadhalika ni njia ya kudhibiti unene, kisukari na mafuta yaliyozidi mwilini na kuepusha shinikizo kubwa la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na saratani.

Aidha ni muhimu kufanikisha kujenga misuli ambayo husaidia kutumia nishati ya ziada na hivyo kuepuka unene kupindukia.

Kuushughulisha mwili kunajenga mifupa imara na unyumbufu wa viungo badala ya kuwa vigumu na hata kukakamaa. Ni njia ya kupunguza msongo wa mawazo na uchovu.

Kadhalika huleta usingizi mnono, kuongeza kinga ya mwili na kuimarisha hisia huku ukiongeza ufanisi wa akili.

Aidha, ni dawa ya kuchelewa kwa mwamko au mlipuko wa dalili za magonjwa ya akili kama sonona na wasiwasi, pamoja na kupunguza dalili nyinginezo za maradhi ya akili.

Kiwango cha mazoezi kinacholeta faida ni shughuli isiyopungua dakika 30 kwa siku angalau siku tano kwa wiki. Hizo dakika 30 zinaweza kuchukuliwa kwa vipindi tofauti.

ELIMU

NA SHABAN NJIA, KAHAMA

# Binti anapotosa mipango ya kuozwa utotoni kisa mahari ya ng'ombe saba na Sh. 200,000

• Wazazi waisoma namba, leo yuko chuoni SUA

KASHINDE Mwendesha (20) ni shujaa aliyeruka na kuchomoka viunzi akiyakimbilia mafanikio ya elimu na sasa ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), akisoma shahada ya maendeleo ya jamii.

Ameishi uhamishoni kwa miaka miwili akijiokoa na balaa la kuozwa na miaka 17 alipomaliza kidato cha nne. Ni ndoa zinazoathiri mabinti vijijini wanaolazimishwa kuolewa licha ya kuwa wadogo kwa kisingizo cha kupata mali au kuenzi mila potofu.

**KILICHOMKUTA KASHINJE**

Akizaliwa katika Kijiji cha Nyikoboko wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, Kashinje anapotimiza miaka 17, anafaulu mtihani wa kidato cha nne kwa kupata daraja la pili, lakini familia yake haikuona umuhimu wa kuendelea na kidato cha sita, ikishawishika na mahari ya Sh. 200,000 na ng'ombe saba.

Kashinje anasema, awali aliweka msimamo pamoja na mama mzazi kuwa lazima atimize malengo ya kielimu afike chuo kikuu, ndipo aolewe. Mama alimuunga mkono na kumsisitiza kuongeza juhudi darasani.

Ni mwishowe, yeye kati ya watoto sita ndiye pekee aliyefaulu kidato cha nne na kuendelea na masomo ya kidato cha tano kwani ndugu zake watano waliishia darasa la saba, kidato cha pili na waliofika kidato cha nne walifeli na kuozwa ili familia inufaike na mifugo na fedha za mahari.

"Famili yetu ina watoto sita, watatu wa kiume na idadi ya wasichana ni watatu pia, kaka zangu wameshaoa kwasababu walishindwa kusoma na wawili walifika kidato cha nne ila wafeli na mmoja aliishia la saba. Dada zangu waliishia kidato cha pili na kuozwa na mwingine aliacha masomo akiozwa ila sikutaka hili linitoke," anasema Kashinje.

Anakumbusha kuwa wakati akisubiri matokeo, mchumba wa kwanza alijitokeza kwa shinikizo la baba yake, aliyemtoza mahari ya ng'ombe 10 na Shilingi 300,000, alivyoshindwa kukidhi kiwango hicho aliondoka, hatua iliyomwongeza ari ya kuendelea na shule.

Kashinje anasema, wiki mbili baadaye alijitokeza wa pili baada ya kuzungumza na wazazi wakakubaliana alipe ng'ombe saba na Sh.200,000. Mama yake hakuwa na sauti hivyo alikubali aache masomo aolewe, lakini kipindi hicho matokeo yalitoka akapata ufaulu wa daraja la pili.

"Sikutaka kuolewa kabisa kwasababu nilitaka kusoma na nilikuwa nimefaulu kwenda kidato cha tano, familia nzima na majirani wanaonizunguka walinishawishi nikubali yaishe ila akili kichwani. Nilionekana binti wa Kisukuma asiye na heshima tena kwa kukataa matakwa ya wazazi wanaona kesho yangu," anasema Kashinje.

Anamtaja mwalimu wake wa sekondari Boniphace Madurya, baada ya kupata taarifa hizo alikwenda kuripoti katika vyombo vya sheria na mama yake alikamatwa na kupelekwa polisi.

Anadai kituoni hapo walihonga Sh.500,000 na kutoka wakiwa na msimamo huohuo hadi Ofisi ya Ustawi wa Jamii ilipoingilia kati na kuzuia ndoa hiyo na kumpeleka kwa mjomba wake anayeishi Mipa Kishapu, mwenye uelewa wa masuala ya elimu.

Anasema kutoka nyumbani kwake alikwenda kusoma kidato cha tano na sita na mwaka 2022 alipohitimu alirejea nyumbani, akipokelewa na sasa yuko Chuo Kikuu SUA.

Anasema shahada anayosoma ni ya maendeleo ya jamii akitarajia kuwa balozi wa kukabiliana na ndoa za utotoni.

**SAUTI YA MAMA MZAZI**

Theresia Bupamba ni mama mzazi wa binti huyo, anakiri walitaka kumwozesha mtoto wao ili kuisaidia familia kuondokana na umasikini.

"Kama unavyojua utajiri wa Wasukuma ni mifugo hasa ng'ombe hivyo nilitakiwa kumshawishi mwananangu akubali kuachana na shule akaolewe," anasema Theresia.

Anaongeza kuwa awali alikuwa akishirikiana na mwanawe kupinga kuozwa kwani ndugu zake walishindwa masomo na kuozwa ndio sababu mchumba wa kwanza alipofika walimtajia mahari kubwa ya ng'ombe 10 na Sh.300,000 ili aondoke ili kumpa nafasi binti yake kusoma kwani alifaulu vizuri.

"Niliposikia amepelekwa kwa mjomba wake hofu yangu ilitoweka nikajua atasoma na kutimiza ndoto zake na ameonyesha ujasiri wa kujisimamia na kuhakikisha haolewi na sasa kiu yake ya kufika chuo kikuu na kusoma kile anachohitaji imetimizwa," anaongeza Theresia.

**MABINTI WANAUMIZWA**

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Msalala, Richard Ng'ondya, anasema, ukatili kwenye jamii umeshamiri kwa kiwango kikubwa na mabinti wanakosa masomo.



Mshindi wa vita ya ukatili wa kijinsia Kashinde Mwendesha.
**PICHA: SHABAN NJIA**

Aidha kwa kushawishiwa na wazazi wasifanye vema kwenye mitihani ya mwisho ili wafeli na kuozwa na wengine kutoroshwa na kutolewa masomoni.

Anasema, binti Kashinje alionyesha ujasiri wa kupambana asiolewe na kuhakikisha anatimiza ndoto zake za kufika chuo kikuu ndio sababu walipopata taarifa za tukio hilo walifika mara moja na kumhifadhi sehemu salama kabla ya kumpeleka kwa mjomba wake huku wakiendelea kuchukua hatua kwa wazazi wake.

Ng'ondya anasema, wazazi wake walipatia elimu ya ukatili wa kijinsia na kwa kuwaeleza kile walichokuwa wanakifanya ni kosa na watakiwa kushtakiwa na kukubali kutoa ushirikiano na kuchangia Sh.700,000 za maandalizi ya kidato cha tano na sita na wakati huo tayari binti yao alikuwa ameshapelekwa kwa mjomba Kishapu.

"Binti huyu ni jasiri na anapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwenye jamii, alijisimamia asiozwe na sasa yuko chuo kikuu, tulipopata taarifa zake tulimhifadhi kwa ofisa maendeleo wa kata yake kwa muda na baadae mimi mwenyewe nilimbeba mpaka kwa mjomba wake anayeishi Mipa-Kishapu na alitokea hapo kwenda Sshule Korogwe-Tanga"Anasema Ng'ondya.

> "Shahada anayosoma ni ya maendeleo ya jamii akitarajia kuwa balozi wa kukabiliana na ndoa za utotoni.

Aidha anasema, kwasasa wana kituo cha huduma ya shufaa kipo kata ya Bugarama na kina daktari, dawati la jinsia na ustawi wa jamii na kwa siku wanapokea mashauri manne hadi sita na kuwataka wananchi kukitumia katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyotokea ili kuvidhibiti.

**WAPAZA SAUTI**

Mwenyekiti wa Wanawake 100,000 Taifa, Anascolastika Ndagiwe, anampongeza binti huyo kwa kuonyesha ujasiri wa kukataa kuozwa, licha ya wazazi wake wanaomzunguka kumkatisha tamaa ya kuwa sio vema kukataa kuolewa na mahari kurejeshwa kwa madai ni kujitafutia mikosa kwenye maisha jambo ambalo si kweli.

Anasema, wazazi wanatakiwa kuwajibishwa kisheria kwa walilotaka kulifanya ili iwe fundisho kwa wengine wenye tamaa ya mali wanaokatisha ndoto za mabinti zao, akiziomba mamlaka zilizomsaidia binti huyo kufuatilia ndugu zake walioozwa kama waliolewa wakiwa na umri sahihi.

Sheria ya Mtoto ya 2009 sura ya 13, kifungu cha nane kifungu kidogo cha pili inawaonya wote wanaomnyang'anya mtoto haki ya kupata elimu, chakula, mavazi, malazi, huduma za afya au kitu chochote kinachohitajika kwa ajili ya maendeleo yake.

Hata hivyo Sheria ya Ndoa 1971 imekuwa na kigugumizi katika kudhibiti ndoa za utotoni na kuzidi kuwapa kiburi wazazi wanaoendekeza vitendo hivyo. Sheria hiyo imewataja wafunga ndoa kuwa ni wale waliotimiza umri wa miaka 18.

Huku ikibainisha kuwa chini ya umri huo iwapo tu kibali kimetolewa na wazazi kwa binti aliye chini ya miaka 15 na mahakama kwa aliye chini ya miaka 14.

Mwanaume anaweza kuruhusiwa na mahakama kuoa akiwa chini ya miaka 18 lakini si chini ya miaka 14 kama ataonyesha kuelewa jukumu lake kama mtu mzima.

ELIMU
NA WAANDISHI WETU

# Mtaalamu anaposisitiza umuhimu mbolea shambani, kuua viuatilifu kwenye udongo

KWA walio wengi kilimo cha mboga ni lazima kuwa na eneo kubwa na lenye nafasi kwa ajili ya kuandaa bustani.

Wakifikiria kuwa kuna kutumia gharama kuliandaa, kununua mbolea, kuandaa vitalu na hata namna bora ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji ikiwamo mifereji na mitaro ya kusambaza maji.

Lakini, sasa unaweza kulima mboga nyumbani kwako, kwa kutumia eneo dogo ulilonalo au kuzipanda kwenye makopo kama unavyopanda maua na makasha mbalimbali.

Kwanza kupunguza gharama ya ununuzi wa mboga za nyumbani, pia zinakuwa salama katika kuandaliwa kwani zinalimwa kwa kuzingatia mbinu sahihi za kupanda na kutunzwa hasa kuepuka kemikali.

Baadhi ya wakulima wanakumbana na changamoto ya namna gani anaweza kuandaa mashamba yao ili wapate mimea yenye virutubisho vya kutosha na kufanya mlaji apate kilicho sahihi.

Hiyo ni kutokana na kukosa elimu sahihi ya kuandaa mashamba na bustani kwa ajili ya kupanda mimea, ndio maana mazao hushindwa kustawi vizuri na wakati mwingine kufa.

Jamii imeshuhudia mazao mengi yakishambuliwa na wadudu, kama vile migomba na mboga hali hiyo inapelekea mkulima au mwenye bustani kurudi nyuma kutokana na mimea kuathiriwa.

Kwa upande wa migomba inabadilika rangi na kuwa ya njano na kuuzuia kuzaa matunda na wakati mwingine mgomba kufa.

Hivyo ili mkulima aepukana na adha za mimea kufa, ni vema kufuata hatua sahihi za kupanda mimea au kundaa mashamba, bustani kwa ajili ya kupanda mazao yenye virutubisho.

Kwa mujibu wa mtalamu wa kilimo, Salimu Hussen, anyeuza pembejeo za kilimo Mwenge jijini Dar es Salaam, baadhi ya wakulima hulima na kupanda mazao, pasipokujua kwenye ardhi hiyo kuna minyoo au virusi vinavyoweza kushambulia mazao yao.

Aidha, anasema mkulima anapoandaa shamba au bustani ni vema akapata elimu sahihi, katika kuandaa kwa kutumia dawa za kurutubisha ardhi na kuua virusi na vimelea waliopo kabla ya kupanda mimea.

Anaendelea kwa kusema ardhi zimetofautiana, kuna ardhi zenye unyevu na zingine hazina hivyo



> Endapo mkulima ataweka mbolea ya chumvichumvi kwenye mboga na kukaa zaidi ya siku tatu kabla ya kuichuma hakuna madhara yatokanayo na mbolea hiyo.

dawa hizo husaidia kuiweka sawa na kuwa na virutubisho tayari kupokea mimea yenye kutoa mazao.

Anakumbusha kuwa mbolea ya samadi inarutubisha udongo, mfano sehemu yenye kichanga inaweza kuirekebisha na kuwa bora yenye rutuba kwa ajili ya mazao mbalimbali.

Ukiachilia mbali mbolea ya samadi ya wanyama, mbolea zilizothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ni muhimu kwa kukuzia mazao kwani zina virutubisho vinavyostahili.

Kwa kutambua hili serikali imeshusha bei ya pembejeo za kilimo kwa kutoa ruzuku, kwa kila mkulima atakayejiunga na kuwa na namba ya usajili atanunua kwa bei ya punguzo ndiyo ruzuku.

Sote tunatambua ili kilimo kiwe bora ni lazima kutumia mbolea na dawa za kuwa wadudu kabla ya kupanda mbegu, hivyo serikali imewarahishia wakulima kwa kuweka punguzo kwenye pembejeo za kilimo.

Mtaalamu wa kilimo Hussen, anasema mfuko wa kilo 50 unatumika kwenye heka moja ya shamba na kujitosheleza kustawisha mimea.

Oktoba 2022, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, anawataka maofisa ugani kuhimiza kufanya operesheni ya kujiwekea malengo, kwamba kwa siku lazima wasajiliwe wakulima 50 katika mfuko wa pembejeo za kilimo.

Ingawa anasema kuwa ana imani inawezekana kusajili wengi zaidi ya hao, hiyo ni kutokana na Watanzania walio wengi ni wakulima na wanatumia gharama kubwa kununua pembejeo za kilimo.

Anayasema hayo kwenye kikao kilichohusisha, wakuu wa wilaya, wakurugezi wa halmashauri zote za jiji pamoja na maofisa ugani wa mkoa huo.

Hivyo kuweka utaratibu wa kuweka bei rafiki ya kununua mbolea yenye ruzuku kwa wakulima, ili kupanua wigo wa kilimo na kuwawekea mazingira ya kuwavutia watanzania kujiwekeza kwenye kilimo.

Mratibu wa Mradi wa FRESH unaoshughulika na kilimo cha mboga wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Mikocheni, Dar es Salaam, Dk. Violeth Mwaijande, anazungumzia matumizi ya mbolea.

|Anasema endapo mkulima ataweka mbolea ya chumvichumvi kwenye mboga na kukaa zaidi ya siku tatu kabla ya kuichuma hakuna madhara yatokanayo na mbolea hiyo.

Mtaalamu huyo anasema kuwa ni vema mkulima akatumia mbolea ya samadi mara ya kwanza, halafu atumie ya chumvichumvi, ili kusaidia mmea kustawi vizuri na kuchocheo kutoa majani mengi.

Pia anaeleza ni vizuri mbolea ya samadi iwe imeoza na sikutumia mbichi ambayo huunguza mimea kwasababu ina moto hivyo haifai kutumiwa, hasa kwenye kilimo cha mboga.

**KUANDAA KITALU**

Utayarishaji wa kitalu cha mboga unajumuisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa shamba mfano usafi kwa kuondoa magugu na vichaka vinavyozunguka.

Kadhalika kuweka dawa ya kuondoa magugu, kwasababu magugu huua mimea, husababisha isiote wala kustawi vizuri kwani inaizingira na endapo mkulima atatumia njia za kisasa anatajipatia mavuno mengi.

Mtaalamu wa kilimo wa TARI, Dk. Violeth anawataka kuhakikisha upatikanaji wa maji, kuweka mifereji, njia za kuleta maji au kuhifadhi maji kwa kutengeneza kisima au matangi.

Anasema ni vizuri kutenga eneo maalumu kwa ajili ya kuhifadhi na kuchanganya mbolea shambani au bustanini.

Vile vile Dk. Violeth anashauri kutifua kwa jembe eneo unalootesha miche, au kusia mbegu pia bila kusahau kuangamiza wadudu na magonjwa yatokanayo na udongo.

Anasema kabla ya kutayarisha matuta ya kitalu ni lazima kutumia dawa ya kunyunyiza katika udongo, kuharibu wadudu waharibifu.

"Unaweza kuchoma udongo au kufunika eneo la tuta la kitalu kwa kutumia plastiki inayopitisha mwanga kwa wiki mbili hadi nne ili kuua wadudu na minyoo udongoni ambayo itapelekea mimea isistawi kikamilifu." Anasema Dk. Violeth.

Anatoa wito kwa wakulima kutumia bustani za maua kwa kupanda mboga na kuachana na dhana kuwa maua yanapendezesha nyumba, kwani mboga pia ni kivutio.

Vile vile inapaswa wafahamu kuwa hata mboga zikipandwa kwa ustadi zinapendezesha nyumba, kuondokana na gharama za kununua mboga masokoni ambazo haifahamiki zilivyoandaliwa.

Dk. Violeth pia anawashauri kutumia mbolea ya chumvichumvi kwani serikali imeweka punguzo la bei ili mkulima amudu mbolea hiyo na kuondokana na dhana ya kuwa mbolea hiyo ina madhara wakati ina virutubisho kwenye mmea.

***IMEANDIKWA NA TUNTULE SWEBE, JOYCE LAMECK***



# Bil. 2.5/- zatengwa kununua vifaa vya kufundishia wenye ulemavu vyuoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa watu wenye ulemavu kwenye vyuo vya elimu ya juu 19 nchini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alisema hayo juzi jijini hapa kwenye hafla maalumu ya chakula cha pamoja kwa watu wenye ulemavu ilioandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu wa kushirikiana na taasisi ya kusaidia wenye ulemavu iitwayo Tfed.

Alisema serikali imendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watu wenye ulemavu kwa kuboresha miundombinu mbalimbali ili kuyafikia makundi yote, wakiwamo wanafunzi kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vya elimu ya juu.

"Katika mwaka huu wa fedha serikali imetenga kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia watu wenye ulemavu katika vyuo 19 ambapo kati ya hivyo kimoja ni kutoka Zanzibar.

"Katika awamu ya kwanza ya mpango huu tutagawa baadhi ya vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kujifunzia na kujifundishia ikiwemo kompyuta mpakato, vishikwambi na vifaa vya kurekodia sauti pamoja na vitu vingine ambavyo vitatumika na wanafunzi wenye ulemavu katika vyuo mbalimbali nchini," alisema Nderiananga.

Aidha, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata stahiki zao zote kama ilivyo kwa makundi mengine nchini.

"Tunaishukuru sana serikali yetu kwa jitihada inazofanya kwetu sisi wenye ulemavu hasa kwenye kuboresha miundombinu ya sekta ya elimu pamoja na mikopo ya asilimia mbili kwa ajili ya wenye ulemavu," alisema.

Alisema watu wenye ulemavu wataendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika jitihada anazozifanya za kuwaletea maendeleo Watanzania.

Vile vile aliwataka watu wenye ulemavu waliojiandikisha kwenye dafatari la wakazi kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika kesho kujitokeza kupiga kura na kuchagua viongozi bora.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwataka watu wenye ulemavu kutumia fursa mbalimbali ambazo zinatolewa na serikali ikiwemo mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri.

Hata hivyo, Senyamule alisikitishwa na baadhi ya watu wenye ulemavu kutumia vibaya fursa ambazo wamekuwa wakipatiwa na serikali.

Alisema: "Baadhi ya watu wenye ulemavu tuliwapatia vizimba kwa ajili ya kufanya biashara kwenye Soko la Machinga lakini wao waliuza vizimba kwa watu wengine, niwaombe kama mtu hataki kizimba arudishe kwa serikali ili tuone namna ya kumpa mlemavu mwingine badala ya kuuza vizimba."

# RC aeleza umuhimu wa elimu ya rushwa kwa vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema midahalo inayofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) mkoani hapa ina umuhimu mkubwa kwa kuwa inagusa kundi la vijana linalotajwa kuathirika na mmomonyoko wa maadili.

Senyamule alisema hayo jana katika mdahalo wa wanafunzi wa vyuo vikuu na vile vya kati uliofanyika jijini hapa chini ya usimamizi wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) pamoja na Tume ya Haki za Binadamu.

Alisema TAKUKURU kuanzisha midahalo hiyo katika wilaya zote mkoani hapa imeonyesha kuwa na tija kutokana na kuleta matokeo chanya kwa kundi husika.

"Nawapongeza sana TAKUKURU Dodoma kwa kuendesha midahalo hii kwa sababu imeonyesha kuwa na tija kwa jamii ikiwamo kundi husika la vijana," alisema Senyamule.

Alisema kundi hilo likielewa madhara ya utoaji rushwa na upokeaji watakuwa mabalozi wazuri wa kuielimisha jamii kuhusu mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo mbalimbali.

Naye Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Dodoma, Victor Swella, alisema sababu ya kuandaa midahalo kwa wanafunzi wa shule na vyuo vikuu ni kuileta jamii karibu na taasisi hiyo ili kusaidia mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema mada iliojadiliwa katika mdahalo huo ni kuhusu ukosefu wa uzalendo unavyochangia ushiriki hafifu kwenye uchaguzi, ambapo majadiliano hayo yanawajenga wanafunzi kupata elimu ya uwelewa.

Swella alisema, "Tunazishukuru taasisi zilizoshiriki kwenye mdahalo huo, lakini pia vyuo sita vilivyoleta wanafunzi kushiriki mdahalo."






Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini (PDPC), Dk. Emmanuel Mkilia, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Njedengwa, jijini Dodoma jana, alizionya kampuni za mikopo kutoa taarifa za wateja wao mitaani kuwa watachukuliwa hatua za kisheria. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wahitimu elimu ya juu watakiwa kujiunga vikundi kupata mikopo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAHITIMU wa vyuo vya elimu ya juu nchini wamehimizwa kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali ili kunufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na serikali kupitia halmashauri.

Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Charles Mwamaja alitoa ushauri huo juzi alipokuwa akizungumza na wahitimu wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP) kwenye mahafali ya 38.

Mwamaja aliwataka wahitimu hao kuungana kwenye vikundi hivyo vya ujasiriamali ili wakope mikopo inayotolewa na serikali itakayo wasaidia kuwapa ajira.

Kadhalika aliwataka wahitimu hao kuhakikisha vikundi watakavyo viunda vinasajiliwa ili kutambuliwa na kupatiwa mikopo.

Alisema wakisajiliwa itakuwa rahisi kuunganishwa na fursa mbalimbali za kiuchumi na kuweza kupata mitaji mikubwa kwa ajili ya kuanzisha miradi itakayo wakwamua kiuchumi.

Aidha, alikipongeza chuo hicho kwa kuwaandaa wasomi hao kwa kuwapatia elimu na maarifa pindi wanapotoka yanawafanya kushughulikia changamoto kwa wana jamii.

Naye Mkuu wa chuo hicho, Profesa Hozen Mayaya, alisema kuwa chuo hicho kimekuwa msaada mkubwa kwa kuwaandaa wataalamu mbalimbali wanaopatiwa mafunzo kwa ajili ya maisha yao na jamiii zao.

Hata hivyo, aliishukuru serikali kwa kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo ya kujifunzia na kufundishia na kuwasaidia wahitimu kuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe.

**Alisema wakisajiliwa itakuwa rahisi kuunganishwa na fursa mbalimbali za kiuchumi na kuweza kupata mitaji mikubwa kwa ajili ya kuanzisha miradi itakayo wakwamua kiuchumi.**





# Dk. Ndumbaro: Msichague viongozi wa ovyo S/mitaa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WANANCHI wa Kijiji cha Image wilayani Njombe wametakiwa kutochagua viongozi wa ovyo kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa sababu hawatapata maendeleo.

Wito huo ulitolewa juzi na Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, wakati akizungumza na wananchi wa kijiji hicho Jimbo la Lupembe wilayani Njombe.

Alisema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni uchaguzi muhimu zaidi kuliko uchaguzi wowote ule na kwamba viongozi wa ovyo wanapatikana kwa wananchi kutokwenda kupiga kura.

"Wengi tunaongelea sana Uchaguzi Mkuu lakini niwaambie, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndiyo uchaguzi mzuri zaidi, ndiyo uchaguzi muhimu zaidi kwa sababu tunakwenda kuwachagua watu, tunakwenda kuwaweka viongozi tunaoishi nao zaidi kuliko wowote wale," alisema Ndumbaro.

Waziri Ndumbaro alisema viongozi hao wa serikali za mitaa ndiyo chimbuko la maendeleo katika maeneo yao, hivyo wanapaswa kushiriki uchaguzi ili kuweza kupata viongozi bora.

"Kama sehemu barabara mbovu, daraja limevunjika, shule hakuna, zahanati hakuna, umeme hauwaki, hakuna maji hawa ndiyo wa kwanza kujua na wanajadili katika ngazi yao na kufikisha juu, hivyo bila ya hawa viongozi hatuwezi kuleta maendeleo," alisema Dk. Ndumbaro.

Aidha, Waziri Ndumbaro alisema Novemba 27 siku ya Jumatano wananchi wote kwa umoja wao wanapaswa kwenda kuchagua viongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji wanaotokana na Chama Cha Mpinduzi (CCM).

"Hilo halina ubishi kwa sababu Rais, mbunge na madiwani ni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) sasa kwenye serikali za vijiji mkalete upinzani atashirikiana na nani, mkileta hao wengine hakuna maendeleo," alisema Ndumbaro.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwin Swalle aliwataka wanachi hao kujitokeza kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili waweze kuchagua viongozi bora watakaoweza kuwapambania.

Swalle alisema katika miaka minne ya Rais Samia Suluhu Hassan wamejenga zahanati mpya zaidi ya 17, shule za sekondari nne, shule za msingi nne.

"Lakini pia tumefukuza giza kwa maana ya kupeleka umeme vijiji vyote 45 vya jimbo la Lupembe kwa sasa vinaumeme lakini hata barabara za TARURA zimeimarika sana," alisema Swalle.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini kote unatarajiwa kufanyika siku ya Jumatano Novemba 27 ambapo Rais Samia Suluhu Hassan ameitangaza siku hiyo kuwa ya mapumziko ili wananchi wapate fursa ya kupiga kura bila ya vikwazo.

## Mtaka awaonya wanachama Isowelo kuacha makundi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewaonya wanachama wa Chama cha Ushirikia cha Isowelo Amcos kilichoko Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuacha makundi, badala yake wajikite katika kutafuta suluhu katika migogoro yao.

Mtaka alitoa agizo hilo juzi wakati alipokuwa akizungumza na wanachama wa Isowelo Amcos ambapo alisema vyama vingi vya ushirikia vinakufa kwa sababu ya ujinga.

"Kama mnaona kuna watu miongoni mwa wanachama hawa wanaturudisha nyuma badala ya kwenda mbele mnapopatarajia waondoeni, ni lazima mwanachama achague moto au baridi," alisema Mtaka.

Mtaka alisema ni vyema wanachama wa chama hicho na viongozi kuzingatia mshikamano na uadilifu katika kusimamia chama hicho.

"Natoa wito kwenu kuacha tofauti za kikundi au binafsi na kujikita zaidi katika maendeleo ya chama na ustawi wa wanachama wenu, ushirika huu unapaswa kuwa mfano wa mshikamano na usawa," alisema Mtaka.

Awali Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Njombe, Edmund Masawe, alisema chanzo cha mgogoro huo ni katika mkutano mkuu bodi iliyomaliza muda wake kulalamika kwamba wanachama hawajatambua mchango wao kwenye chama kipindi cha uongozi wao.

Mmoja wa wanachama wa Amcos hiyo, Mathias Mwane alisema mgogoro huo umesababisha wakulima kushindwa kuanza shughuli za kilimo, hali ambayo inaweza kuwasababishia kuwa masikini.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Isowelu, Elia Mhonjwa alisema baada ya kuona mgogoro huo unakuwa siku hadi siku ilimlazimu kutaka kujiudhuru.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Fani Mussa, akifungua mafunzo kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii awamu ya kwanza jana, washiriki 238 wamepokelewa katika vyuo mbalimbali vya afya na sayansi shirikishi wilayani hapo kwa ajili ya mafunzo hayo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vibaka wawanyima usingizi wakazi Buguruni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Mtaa wa Buguruni Kata ya Njombe Mjini mkoani Njombe, wamelalamikia uwepo wa vibaka ambao wamekuwa tishio katika usalama wao.

Hivyo wamewataka viongozi watakaoshinda katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwenda kuweka mkakati wa kupambana nao.

Wananchi hao akiwamo, Anna Msigwa walitoa kilio hicho juzi kwenye mkutano wa kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wakati mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wajumbe wake wakinadi sera zao na kwamba vibaka wamekuwa kikwazo kwao.

"Wakati mwingine unaamka asubuhi kwenda kwenye mihangaiko au unasafiri unakuwa na hofu kwa sababu mtaa huu vibaka wamekithiri hata majumbani wanaingia na kufanya udokozi," alisema.

Naye Maneno Ilomo alisema wanataka kuchagua kiongozi ambaye anaweza kuwadhibiti vibaka kwa sababu wamekuwa wengi wanaiba na kuvunja nyumba pindi tu tunapotoka kwenda shambani.

Kwa upande wake, mgombea nafasi ya Mwenyekiti Mtaa wa Buguruni, Hekima Mhagama (CCM), alisema suala la ulinzi na usalama katika mtaa huo ni kipaumbele cha kwanza kwake na hivyo atakwenda kukutana na vijana kuweka mkakati wa pamoja wa kukabiliana endapo watamchagua.

"Mkinichagua tunaweza kuyafanyia kazi kwa pamoja eneo la kwanza ni ulinzi na usalama kwa kushirikiana na vijana wenzangu tunaweza tukaufanya mtaa wetu wa Buguruni ukawa salama," alisema Mhagama.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete, alisema Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imeendelea kutekeleza miradi mingi ya mabilioni ya fedha na kwamba vyama vya upinzani vinapaswa kuendelea kuwakumbusha pale wanaposahau kutekeleza.

Mpete alisema katika kipindi cha miaka iliyopita Kata ya Njombe Mjini imetekelezwa miradi ya zaidi ya Sh. bilioni mbili na hivyo endapo wananchi watawachagua wenyeviti na wajumbe wanaotokana na CCM itakuwa rahisi kuendelea kupata fedha nyingine za kutekeleza miradi mipya.

Diwani wa Kata ya Njombe Mjini, Alatanga Nyagawa, alisema tayari Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo mengi na hivyo ili mambo yaendelee vyema ni muhimu kukipigia kura chama hicho ili kukamilisha kazi.

Wakati huo huo, mgombea nafasi ya Mwenyekiti katika Mtaa wa Buguruni (CHADEMA), Emmanuel Ngelime alisema suala la mapambano dhidi ya vibaka ni miongoni mwa ajenda zake kuu katika mtaa huo.





## Sera ya majisafi, taka kuongeza upatikanaji maji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi amesema kuanzishwa kwa sera ya majisafi na majitaka visiwani Zanzibar kutaongeza upatikanaji wa huduma hiyo kwa wingi visiwani humu.

Alisema hayo wakati akifungua kikao cha wadau wa maendeleo wa sekta ya maji visiwani hapa.

Alisema kwa mara ya kwanza Zanzibar imeona haja ya kuanzishwa kwa sera hiyo ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kuwa ya ubora mjini na vijijini kwa upande wa Kisiwa cha Unguja na Pemba.

Alisema kuwa maji hayo yatakuwa yakitumika kwa ajili ya upande wa kumwagilia ili wakulima na watu wengi kutumia maji hayo.

Alisema kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa upande wa Zanzibar inazidi kuimarika kwa vile kuna miradi mbalimbali.

Alisema kuwa katika kikao hicho wataalamu wa maji kutoka Zanzibar watapata nafasi ya kuzungumza hali ya upatikanaji wake pamoja na changamoto zinazoikumba sekta hiyo.

Kadhalika alisema katika kikao hicho wadau wa sekta hiyo wanaweza kuona maeneo gani wanaweza kuongeza nguvu katika sekta hiyo na kuendelea kupata maendeleo zaidi kwa Zanzibar.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Dk. Salha Mohamned Kassim, alisema kuwa kikao hicho kinalengo la kujadili hali ya upatikanaji wa huduma hiyo ya maji ili kuona huduma hiyo inapatikana wakati wote.

Alisema kuwa kuanzishwa kwa sera ya majitaka inakwenda kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma hiyo kirahisi zaidi na wizara imejipanga kuona jambo hilo linafanikiwa kwa kiwango kikubwa.

# Serikali kuchukua hatua kumaliza ajali barabarani

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali inaendelea kuchukua hatua pamoja na kutekeleza mkakati wa usalama barabarani, ili kuhakikisha inaondoa vifo visivyokuwa na lazima pamoja na ulemavu wa kudumu kwa wananchi.

Alisema hayo juzi katika hafla ya kilele cha maadhimisho ya kwanza ya wiki ya usalama barabarani na uzinduzi wa mkakati wa usalama barabarani Zanzibar.

Alisema kuwa kila mmoja ana jukumu la kuhakikisha ajali za barabarani zinapungua na kuondoka kabisa kwa kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara yatokanayo na ajali hizo ikiwamo vifo na ulemavu wa kudumu.

Alisema utafiti unaonesha kuwa chanzo kikubwa cha ajali za barabarani zinatokana na makosa ya kibinadamu yanayo sababishwa na madereva kutokufuata sheria za usalama barabarani, kutembea kwa mwendokasi, ulevi, kutumia simu wakati wanaendesha magari, ubovu wa magari, uchakavu wa miundombinu ama hali ya hewa.

Alisema jamii inapaswa kutumia utafiti hizo ili kusaidia kuonesha chanzo cha tatizo na namna ya kutatua, ikiwemo la ajali za barabarani zinazoendelea kugharimu maisha ya watu na mali zao.

Hemed alisema kuwa takwimu zinaonesha kuanzia mwaka 2019 hadi 2023 ajali za barabarani 1,181 zimeripotiwa kwa vyombo husika zilizosababisha vifo 799 na majeruhi 1,461.

Alisema kuanzia Januari hadi Oktoba 2024 ajali 193 zimeripotiwa na kusababisha vifo 264 na majeruhi 216.

Hivyo, aliitaka Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kisheria ikiwamo kutoa elimu kwa jamii.

Pia alilitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha sheria za usalama zinafuatwa kikamilifu na kuwachukulia hatua wale wote wanaokwenda kinyume na sheria hizo.

Kadhalika, aliwataka madereva kufuata sheria za usalama barabarani na kuhakikisha uimara wa vyombo vyao kabla ya kuingia barabarani pamoja na wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vinavyosimamia usalama.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed, alisema ajali za barabarani ni janga la taifa linaloendelea kupoteza maisha ya wananchi kupata ulemavu wa kudumu pamoja na upotevu wa mali zao.

Dk. Khalid alisema ushirikiano wa pamoja unahitajika katika kuhakikisha kila mmoja anafuata sheria za usalama barabarani, kutolewa elimu ya matumizi ya usalama barabara ili kumaliza kabisa janga hilo.

Alisema kuwa katika harakati za kupambana na kupunguza ajali za barabarani lazima kuwapo na mazingatio ya mipango miji ambapo wimbi la ujenzi holela hasa pembezoni mwa barabara jambo ambalo linachangia kuongezeka kwa ajali.

Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alipongeza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi za kuleta maendeleo hasa katika sekta ya miundombinu ya barabara na kuakisi dhamira yake ya kuimarisha usalama barabarani.

Alisema pia anampongeza kwa kutokomeza kabisa ajali zinazosababishwa na madereva, wamiliki na wananchi kutokufuata sheria za usalama barabarani.

Kamishna Hamad alisema Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo watumiaji wa barabara kutokuwa na elimu ya usalama barabarani.

Hivyo, alishauri kuendelea kutolewa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi bora ya barabara na kufuata sheria za usalama barabarani.



Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya jeshi hilo, Kilimani Mjini Zanzibar, kuhusu Siku 16 za Kupinga Udhalilishaji wa Kijinsia jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaharakati wanaopinga udhalilishaji kupewa tuzo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) inatarajia kutoa tuzo kwa wanaharakati vinara na mashirika ambayo yameonyesha juhudi na ushujaa katika kupinga matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

Hafla hiyo ya utoaji tunzo inatarajiwa kufanyika Desemba saba mwaka huu, kwamba lengo ni kuwathamini, kuwatambua, kuwaunga mkono na kuwapa heshima mashujaa waliojitolea kuhakikisha Zanzibar inakuwa mahali salama kwa wanawake na watoto kwa kutambua, kuripoti na kuzuia matukio ya udhalilishaji, kujenga utamaduni wa kuheshimiana na uwajibikaji.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa ZAFELA, Jamila Mahmoud, alisema safari ya kukomesha ukatili wa kijinsia inaanza na kila mmoja, hivyo tuzo hizo ni nyenzo muhimu ya kuleta mabadiliko katika jamii.

Hivyo, aliwataka wananchi, viongozi wa jamii na watunga sera kuunga mkono juhudi hizo kwa kushiriki katika matukio ya kupinga udhalilishaji wa kijinsia na kufanya uchechemuzi wa sera zinazolinda waathirika na kuwaadhibu wahusika.

Aidha, alitaka jamii kuungana katika kuhamasisha ulezi, utetezi na mabadiliko ya kudumu ili kudhibiti vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema utoaji wa tuzo hiyo unakwenda sambamba na maadhimisho ya siku 16 za kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema katika kupinga siku 16 za kupinga udhalilishaji Zafela imeandaa siku maalumu ya kuwatembelea na kuwafariji wafungwa wa kike waliopo gerezani pamoja na utoaji wa elimu kwa mikoa yote ya Zanzibar kuhusu udhalilishaji wa kijinsia.

Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alisema Jeshi la Polisi Zanzibar linasimama mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa kesi za ukatili wa kijinsia zinashughulikiwa kwa haraka na haki inapatikana kwa waathirika.

Hivyo, aliitaka jamii kushirikiana kwa karibu na vyombo vya sheria kwa kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili vinavyofanyika nyumbani, shuleni, kazini na katika maeneo ya umma na kitendo cha kukaa kimya ni kushiriki katika kuendeleza ukatili.

KESI YA KUCHOMA MKE

# Ripoti za ugonjwa wa akili zaleta utata

Na Grace Gurisha

KESI ya mauaji inayomkabili Khamis Luwongo (38) anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kisha kuuchoma moto mwili wake imechukua sura mpya, baada ya Mahakama kupokea ripoti mbili zenye majibu tofauti ya akili kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili, Mirembe.

Ripoti ya kwanza iliyotumwa kwa njia ya mtandao kutoka hospitali hiyo ilieleza kuwa wakati mshtakiwa anatenda kosa hilo hakuwa timamu kiakili, lakini ripoti iliyoletwa mkononi na daktari aliyeandaa inaeleza wakati wa tukio alikuwa timamu.

Hali hiyo iliyotokea jana mbele ya Jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati Daktari Bingwa wa Afya ya Akili, Dk. Sadiki Mandari kutoka Mirembe akijibu maswali ya jaji, maswali ya jopo la mawakili wa serikali na maswali ya Wakili wa utetezi, Hilda Mushi.

Sintofahamu hiyo ilijitokeza, baada ya Wakili Mushi kupinga kupokewa ripoti hiyo kama kielelezo kwa sababu ipo tofauti na ya awali katika hitimisho, huku Dk. Mandari akinyoosha nyaraka hiyo juu na kudai kuwa hiyo ndio nyaraka halisi (original) aliyokuja nayo yeye.




Mfanyabiashara Khamis Luwonga (katikati) anayetuhumiwa kumuua mke wake na kisha kuchoma mwili wake kwa magunia ya mkaa akiongozwa na askari mahakamani akienda kusikiliza kesi yake.

Hata hivyo, Mahakama hiyo ilipokea kielelezo hicho na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mwasiti Athuman aliendelea kumuuliza maswali shahidi na kumwelekeza asome sehemu ya nyaraka hiyo ambayo inaonesha kwamba mshtakiwa siku ya tukio alikuwa timamu.

Daktari alisoma kwa sauti ripoti hiyo ya Septemba 26, 2024 kuwa mshtakiwa hakuwa na shida yoyote na hata alivyopokewa Mirembe hakuwa na hali mbaya alikuwa ana uwezo mzuri wa kufanya uamuzi.

Wakili wa Serikali, Ashura Mzava kwa nafasi yake alimpatia nyaraka zote na kumwelekeza akaangalie sehemu ya muhuri na saini, akidai kwamba kuna tofauti saini hazifanani, haitambui hiyo nyaraka.

Pia, daktari huyo alidai kuwa mshtakiwa Luwongo hakumweleza chochote kuhusu yeye kupata giza na wakati anatenda tukio hilo alikuwa timamu, pia alikuwa anafahamu ripoti kutumika mahakamani na hajawahi kukutana na ndugu yeyote wa mshtakiwa.

Wakili wa utetezi, Mushi alipewa nafasi ya kumuuliza maswali shahidi kutokana na ripoti mbili alizoziandaa na kisha kuikataa moja ambayo ilitumwa na hospitali hiyo moja kwa moja mahakamani na kudai kuwa aliyokuwa nayo mkononi ndio halisi.

**Mushi: Kuna ripoti ambayo ililetwa mahakamani moja kwa moja kutoka Mirembe, soma kwa sauti chini hapo kwenye muhuri kuna jina la nani?**

**Dk. Mandari:** Dk. Sadiki Mrisho Mandari.

**Mushi: Soma mstari wa mwisho wa hitimisho inasema nini?**

**Dk. Mandari:** Kwa mujibu wa hii nyaraka siku mshtakiwa anafanya tukio hakuwa timamu kiakili.

**Mushi: Ulionana na mshtakiwa mara moja ni kweli kama nilivyokusikia.**

**Dk. Mandari:** Ni kweli

**Mushi: Ugonjwa alionao mshtakiwa anaweza kuchanganyikiwa?**

**Dk. Mandari:** Anaweza.

**Mushi: Hali hiyo ya ugonjwa wa kifafa ambao katika uchunguzi wenu mlibaini, wakati yupo Mirembe ilimtokea?**

**Dk. Mandari:** Ndiyo

**Mushi: Ripoti uliyokuja nayo inatofautiana na ripoti iliyotumwa mahakamani kwenye hitimisho.**

**Dk. Mandari:** Ndio zinatofautiana.

**Jaji: Wewe msomi kabisa umetuvuruga, kwanini umekuja na taarifa mbili na unajua kabisa hapa inayotafutwa ni haki.**

**Dk. Mandari:** Mmeniapisha niseme ukweli, hii nyaraka nimeitoa Masjala ya Hospitali ya Mirembe.

**Jaji: Ni sawa hata hii imetoka Masjala, 'why' (kwanini) zipo mbili bana na wewe ni msomi kabisa 'why'?**

**Dk. Mandari:** Ndugu wa mshtakiwa alinipigia simu kwamba ripoti zipo mbili, aje kuitetea iliyokuwapo mahakamani, namba yake sikuisevu wala siijui.

**Jaji: Yeye alijuaje kama kuna ripoti nyingine na kama wewe unakuja kuzizungumzia.**

**Dk. Mandari:** Mimi sikumwambia kuhusu ripoti, lakini sijui yeye.

"Akasema kama inawezekana kesho (jana) tuonane, mimi ninajua ninachokifanya na nimesoma," alidai Dk. Mandari.

**Jaji: Wewe ni msomi 'why' unakuja na hizi taarifa mbili, hapa kuna maisha ya mtu yamepotea halafu wewe unafanya vitu vya namna hii kweli?**

**Dk. Mandari:** Angalia kwenye Tigopesa utaona ni nani? Au ngoja nimpigie hapa hapa, akapiga huku akiwa ameweka 'loudspeaker' (sauti) ikawa inaita.

**Jaji: Mwenye simu apokee, nimetoa ruhusa hiyo, lakini haikupokewa.**

**Dk. Mandari:** Ngoja nimtumie fedha ili tupate jina lake, akatuma akasema jina linatokea ni dada wa Luwongo.

**Jaji: Yupo humu ndani? Hicho cheo cha Mkurugenzi wa Huduma Tiba ulikipata lini?**

**Dk. Mandari:** Julai.

Wakili wa Serikali Mkuu, Yasinta Peter, aliomba mahakama yote yalikuwa yakiendelea yaingie kwenye rekodi za mahakama.

Pia, aliomba mahakama ifanye majumuisho ya mwisho ya mashahidi ili waweze kufikia haki. Kabla ya mahakama kupanga tarehe mshtakiwa aliomba azungumze kidogo.

"Ni aibu kubwa kwa taasisi inayoaminika na serikali kuleta taarifa mbili na taarifa ya kwanza ilitumwa kwa njia ya mtandao sio askari alibeba mkononi akatembea nayo, daktari anakuja nayo nyingine mkononi anasema ndiyo bora zaidi, hofu yangu hawa mawakili wanaweza wakaleta ripoti nyingine ya mkemia na kuonesha yale majivu ni ya Naomi," alidai.

Hata hivyo, Jaji alimtoa wasiwasi kwa kumweleza kwamba yeye ndio anajua kama anahusika au la, kwa hiyo mahakama itatoa uamuzi.

Alisema majumuisho ya mwisho kwa pande zote watawasilisha mahakamani Desemba 10, 2024 na kesi itatajwa Desemba 11, 2024, siku hiyo ni tarehe ya hukumu kutajwa.

Mshtakiwa Luwonga, mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimuua Naomi Marijani kwa kumchoma moto kwa magunia mawili ya mkaa.


IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
DEEP POLL
(THE REGISTRATION OF DOCUMENTS CAP 117)

**BY THIS DEED, I ELIKA WILLIAM SOKOLO** a citizen of united republic of Tanzania by birth **DO HEREBY ABSOLUTELY** renounce, relinquish and appears in my birth certificate the reason adopted the name is to appear in my **NATIONAL IDENTIFICATION AUTHORITY (NIDA) the name of ELIKA WILLIAM ALEX.** And, in pursuance of such of name as aforesaid I hereby declare that I shall be known, sign at all material times and place hereinafter, in all actions and proceedings, deeds and instruments and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **ELIKA WILLIAM SOKOLO** as my name in lieu of the said former names of **ELIKA WILLIAM ALEX**

And I hereby authorized and request all person to designate, describe and address me by such assumed name of ELIKA **WILLIAM SOKOLO IN WITNESS WHERE OF** I have here under signed my assumed name of **ELIKA WILLIAM SOKOLO**



SIGNED and delivered at Mbeya by
The said ELIKA WILLIAM SOKOLO
Who is known to me personally in my presence
This 22 Day of 11 2024

E. william
ELIKA WILLIAM SOKOLO

BE FORE ME:
NAME MICHAEL JOHN MWAIPASI
SIGNATURE
ADDRESS 4153 MBEYA
QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA RUNGWE
KITUO CHA KIWIRA
SHAURI LA NDOA/TALAKA NA: 32/2024

EZEKIEL BETHANIA CHENGULA.................. MDAI
KISSA SANGA..........................................MDAIWA

HATI YA KUITWA SHAURINI

Mdaiwa KISSA SANGA popote ulipo unaamriwa uhudhurie Mahakamani tarehe 18/12/2024 saa tatu asubuhi bila kukosa. leleweke kuwa usipohudhuriwa siku hiyo shauri linaweza kusikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa pasipo uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 25/11/2024.

PRIMARY COURT AT KIWIRA RUNGWE TANZANIA

Ibrahim Nganico Nganiko
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIWIRA



KUPOTEA KWA VYETI



**JANETH KUYELA KIJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3343-0018** kilichotolewa na JIJA SECONDARY mwaka 2022. Cheti cha darasa la saba chenye namba **PS2705037-070** kilichotolewa na Shule ya Msingi JIJA – 'A' mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/NANE/RB/787/2024.**



JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA
UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI
SHAURI LA MIRATHI NA 29490 YA MWAKA 2014

NAOMBA YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA
LUCY JOSEPH MSOFFE............................MAREHEMU
JOSEPH INNOCENT MKOMBA...................MUOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 11 Mwezi DISEMBA, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 21 Mwezi NOVEMBA Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

DISTRICT COURT

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Hali tete uhasama wa Israel na Lebanon

**TEL AVIV,** Israel

JESHI la Israel limesema kundi la wanamgambo wa Hezbollah limerusha makombora 340 na ndege zisizo na rubani kwenda Israel, na kujeruhi watu 11 na kusababisha madhara makubwa huko Tel Aviv, wakati wapiganaji wake wakiweka upinzani mkali kusini mwa Lebanon.

Aidha, ilielezwa jana kuwa uhasama kati ya mataifa hayo imekuwa kama mchezo wa piga nikupige, kwa kuwa saa chache baada ya mkasa huo kulibainishwa kwamba mashambulizi ya anga ya Israel kwenye mji mkuu wa Lebanon yanaendelea.

Pia ilielezwa kuwa mashambulizi hayo yalisababisha maangamizi makubwa huku Wizara ya Elimu ya Lebanon ikisimamisha wanafunzi kwenye shule huko Beirut hadi Januari, mwakani.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Lebanon mashambulizi ya Israel yaliua takriban watu 84 na kujeruhi 213, ikiwa ni pamoja na 30 ambao waliuawa katika mgomo kwenye jengo la ghorofa katika kitongoji chenye wakazi wengi katikati mwa Beirut.

Katika hatua nyingine, ilielezwa kuwa jumla ya watu 3,072 wameuawa na 13,426 wamejeruhiwa tangu Israel ilipoongeza kampeni yake dhidi ya Hezbollah mnamo Septemba 16, kulingana na takwimu za Wizara ya Afya ya Lebanon.

Wakati hayo yakiendelea, chanzo cha kikanda kilisema mkataba wa kusitisha mapigano kati ya Israel na kundi uko karibu, licha ya ongezeko la mashambulizi ya Israel yanayosababisha idadi ya vifo nchini Lebanon tangu katikati ya Septemba, mwaka huu.

Takwimu za Wizara ya Afya ya Lebanon ilisema zaidi ya watu 3,000 wameuawa katika mashambulizi ya Israel tangu kuzuka kwa mapigano katikati ya mwezi Septemba, huku ikisisitiza udharura wa mpango wa kusitisha mapigano.

Chanzo cha kikanda kilidokeza kuwa ingawa mpango huo ulikuwa karibu zaidi kuliko awali, bado haujaundwa kikamilifu, huku maofisa wa Marekani na Israel wakitahadharisha kuwa bado hakuna mwanga wa kijani uliotolewa kwa wapatanishi.

"Tunaelekea upande huu, lakini bado kuna masuala kadhaa ya kushughulikia," msemaji wa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu aliiambia CNN.

Katika siku za hivi karibuni Hezbollah imekuwa ikizingatia pendekezo la Marekani na Israel la kusitishwa kwa siku 60 katika mapigano ambayo baadhi ya matumaini yanaweza kuwa msingi wa usitishaji vita wa kudumu.

Hata hivyo, Israel ilianzisha mashambulizi makubwa nchini Lebanon katikati ya Septemba kufuatia miezi kadhaa ya mashambulizi ya mpakani ambayo yalianza wakati Hezbollah ilipoishambulia Israel kwa mshikamano na Hamas na Wapalestina huko Gaza.

Vile vile, ilielezwa kuwa tangu wakati huo, Israel imeanzisha uvamizi wa ardhini, na kuua msururu wa viongozi wa Hezbollah ikiwa ni pamoja na mmoja wa waanzilishi wake, Hassan Nasrallah na kujeruhi maelfu ya watu katika shambulio lililowashirikisha waimbaji wa kurasa zinazolipuka. **CNN, Aljazeera**

## Nchi 175 kujadili mkataba wa plastiki

**SEOUL,** Korea Kusini

WAWAKILISHI na wapatanishi kutoka nchi 175 wamekutana mjini Busan, Korea Kusini katika jitihada ya mwisho ya kuandaa mkataba wa kushughulikia mgogoro wa uchafuzi wa plastiki duniani.

Ilielezwa kuwa wawakilishi hao walikutana jana ikiwa ni saa chache baada ya kukamilika kwa mkutano wa kimataifa kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa COP29 uliofanyika huko mjini Baku, Azerbaijan.

Ilielezwa kuwa hiyo ni mara ya tano mataifa ya dunia yanakutana kuandaa mkataba wenye mafungamano ya kisheria.

Mbali na wajumbe wa mataifa tofauti, wawakilishi kutoka sekta ya utengenezaji wa plastiki, wanasayansi na wanamazingira wanahudhuria pia mkutano huo ili kuchangia mawazo kutafuta njia ya kulishughulikia tatizo linaloongezeka la uchafuzi unaotokana na plastiki.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) Inger Andersen alisema sayari ya dunia inayongwa na plastiki, huku maziwa, mito, bahari na miili ya binadamu ikiathiriwa na uchafuzi wa plastiki.

"Tatizo hili linaweza kutafutiwa ufumbuzi na lazima suluhisho lipatikane katika mkutano wa Busan," alisema Andersen. **DW**





Sehemu ya watu 490,000 waliokimbia makazi yao nchini Malawi baada ya kuharibiwa na kimbunga Freddy, ambacho kimelikumba taifa hilo na kusababisha vifo vya watu 476 na 918 kujeruhiwa, huku shirika la kudhibiti majanga likisema wengine 349 hawajulikani waliko. **PICHA: MTANDAO**

## Nyumba za kupanga, waganga wa kienyeji watumika dawa za kulevya

**Na Zanura Mollel**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema inashikilia gari aina ya Scania lenye namba ya usajili wa Afrika Kusini LN87XJPG kwa madai ya kuingiza dawa za kulevya nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo alisema kuwa katika operesheni iliyofanyika Novemba 14-19 mwaka huu, walikamata tani 2.2 za dawa za kulevya katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga sawa na kilogramu 2,207.56.

Alifafanua kuwa kati ya dawa hizo, skanka ni kilogramu 1,500.6, Methamphetamine kilogramu 687.76, heroin kilogramu 19.20 na chupa 10 za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Fentanyl.

"Katika Mtaa wa Pweza Sinza E, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, mtuhumiwa Iddy Mohamed Iddy (46), mkazi wa Chanika Buyuni, alikamatwa akiwa na kilogramu 150.2 za skanka zilizokuwa zimefichwa katika maboksi ya sabuni na baadhi ya dawa hizo zikiwa zimehifadhiwa katika boksi lililotengenezwa kwa bati gumu na kupachikwa kwenye chassis ya gari hilo," alisema Kamishna Lyimo.

Alisema wafanyabiashara wa dawa za kulevya wamebadili mbinu ya kuhifadhi dawa hizo kwa kupangisha nyumba na kuzigeuza ghala la dawa za kulevya, lengo likiwa ni kukwepa kukamatwa.

Kamishna Lyimo alieleza kuwa katika wilaya ya Kigamboni, mtaa wa Nyangwale, watuhumiwa Mohamed Sulieiman Bakar (40) na Sullesh Mhailoh (36), wote wakazi wa Mabibo, walikamatwa wakiwa na kilogramu 1,350.4 za dawa za kulevya aina ya skanka.

"Dawa hizo zilikuwa zimefichwa ndani ya nyumba aliyokuwa amepanga mtuhumiwa Mohamed, ambayo alitumia kama ghala la kuhifadhi dawa hizo, dawa nyingine zilipatikana ndani ya gari aina ya Nissan Juke lenye namba za usajili T 534 EJC, zikiwa tayari kwa kusambazwa," alisema Kamishna Lyimo.

Alisema kuwa katika jiji la Tanga, watuhumiwa Ally Kassim Ally (52) na Fahad Ally Kassim (36) walikamatwa mtaa wa Mwakibila wakiwa na kilogramu 706.96 za dawa za kulevya aina ya Heroin na Methamphetamine, baadhi ya dawa hizo zilipatikani ndani ya gari aina ya Noah lenye namba za usajili T 714 EGX huku nyingine zikibainika kufichwa katika nyumba aliyopanga mtuhumiwa.

Katika Mtaa wa Kipata na Nyamwezi, Kariakoo jijini Dar es Salaam, alisema watuhumiwa Michael Dona Mziwanda (28), mkazi wa Tabata Segerea na Tumpale Bernard Mwasakila (32), mkazi wa Temeke Mikoroshini, walikamatwa wakiwa na chupa 10 za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Fentanyl wakiwa nazo katika duka la M-PESA.

Alisema dawa zilizokamatwa kwa mwezi Novemba pekee ni tani 3.2, na zingeweza kuleta madhara kwa jamii na taifa kama zingeingia mtaani.

Alitoa rai kwa wamiliki wa nyumba kuwa makini wanapopangisha nyumba zao kwa kuwa nyumba inayotumika kwa shughuli za dawa za kulevya ni kinyume inataifishwa kwa mujibu wa sheria, pia mmiliki anapaswa kutoa taarifa anapobaini kuna uhalifu unatendeka katika nyumba yake. Kutofanya hivyo ni kosa la jinai.

# KUKAYE MOTO WAITANGAZA VIZURI ROYAL TOUR UJERUMANI

Na Mwandishi Wetu

KUNDI la muziki la Kukaye Moto Culture Central (KMCC) kutoka nchini Tanzania, Novemba 16, mwaka huu, lilipata nafasi ya kutumbuiza nchini Ujerumani na kutangaza utalii, katika onesho kubambe la African Festival lililofanyika katika mji wa Kemnat na kuhudhuriwa na watu wengi wakiwamo viongozi wa serikali ya mji huo.

Akizungumza na Nipashe akiwa jijini humo, Mkurugenzi wa KMCC, Arba Manillah, alisema kundi hilo lilikuwa likitekeleza kauli mbiu ya maneno na vitendo vilivyooneshwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kuhusu kutangaza utalii na vivutio vya Tanzania.

**Alisema mbali na muziki, wanamuziki wa kundi hilo walitangaza utamaduni, vivutio na mavazi ya Tanzania.**

"Lilikuwa tamasha zuri la African Festival lililofanyika nchini Ujerumani kwenye mji wa Kemnat, Tanzania ilipata mwaliko, lakini kwa sababu zisizoweza kuzuilika, halikwenda kundi lote la Kukaye Moto Culture Central, bali liliwakilishwa na watu wawili ambao ni Bboy Gaga ambaye ni mwalimu wa staili ya uchezaji ya 'Brake Dance' na Don Talent ambaye ni mwalimu wa 'Afro Dance'.

"Kwa bahati nzuri Watanzania wengi wanaishi nchini humo walishiriki tamasha hilo na walituunga mkono mwanzo hadi mwisho wa onyesho," alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema mbali na kundi hilo, onyesho hilo lilishirikisha bendi na vikundi mbalimbali barani Afrika na dunia nzima ambavyo navyo vilipata nafasi ya kuburudisha na kutangaza utalii wa nchini mwao.

"Kingine ambacho kimetupa sifa ni kwamba tulipata nafasi ya kuwafundisha watoto, wanafunzi shuleni kucheza na kuimba, hasa kwa lugha ya Kiswahili ambayo waliifurahia," alisema Manillah, huku akiweka wazi kuwa kundi hilo linatarajia kuwasili mwishoni mwa mwezi huu.



Msanii wa Kundi la Kukaye Moto Culture Central (KMCC), Bboy Gaga, akicheza jukwaani katika onesho la African Festival, lililofanyika hivi karibuni mjini Kemnat, Ujerumani. **PICHA: KMCC**

## *Prisons kusajili wazoefu wa Ligi Kuu Bara dirisha dogo*

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kipigo cha bao 1-0 ilichokipata juzi dhidi ya JKT Tanzania, Kocha Mkuu wa Prisons, Mbwana Makata, amesema anasubiri kipindi cha dirisha dogo ili asajili wachezaji wazoefu wa Ligi Kuu kwani ndicho kinachoitesa timu yake kwa sasa.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa 'Dabi ya Maafande', uliopigwa Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, Makata alisema kwa sasa timu yake ina wachezaji wengi vijana, ambao pamoja na kuwa na vipaji, lakini wanakosa uzoefu na ufanisi.

Alisema kukosekana kwa wachezaji wengi wazoefu kama kina Samson Mbangula, Nurdin Chona na wengine ambao ni majeruhi kunaiathiri kwa kiasi kikubwa timu yake.

"Kuwakosa wachezaji kama Mbangula, Chona nayo ni moja ya sababu ya kupoteza si mechi hii tu hata zingine nyuma kwa sababu ni wachezaji wazoefu, tunawaowatumia kwa sasa wengi ni chipukizi, wana vipaji lakini ufanisi wao ni mdogo kutokana na kukosa uzoefu.

"Nadhani tunaangalia dirisha dogo ili tusajili baadhi ya wachezaji wazoefu kidogo kwenye ligi waje wasaidiane na hawa vijana," alisema kocha huyo.

Akiuzungumzia mchezo huo, Makata alisema walifungwa bao la mapema, na hii sasa imekuwa kama ni ugonjwa kwao, huku wakishindwa kutumia nafasi nyingi walizozipata.

Ahmad Ally, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, alionesha kufurahi timu yake kurejea tena uwanja baada ya muda mrefu na kupata ushindi.

Timu hiyo imerejea dimbani baada ya kukaa nje kwa siku 29, kutokana na wachezaji wake kupata ajali jijini Dar es Salaam, basi la timu hiyo lilipopinduka Oktoba 30, mwaka huu na kusababisha majeruhi kwa wachezaji 11, huku Bodi ya Ligi ikisimamisha michezo yake kutoa fursa ya matibabu.

"Nawapongeza wachezaji wangu, haikuwa rahisi, ilikuwa ni moja ya mechi ngumu kwetu, lakini tumefika ndani ya eneo la mpinzani zaidi ya mara nane, tumepata bao moja, lakini nimefurahi kwa jinsi tulivyokuwa tunashambulia, licha ya kwamba tuna muda mrefu hatujacheza mechi," alisema.

Kwa matokeo hayo, JKT Tanzania imefikisha pointi 13, ikiwa nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikifikisha michezo 10, Prisons ikishuka nafasi moja chini hadi ya 12, ikisalia na pointi 10, kwa michezo 11 iliyocheza.

## TFS kujenga viwanja vya michezo

Na Oscar Assenga, TANGA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wameweka bayana mpango wao kujenga viwanja vya michezo katika maeneo ya Kanda Saba na Shamba la Miti Sao Hill.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Kamishna Msaidizi wa TFS, Erasto Luoga, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Tanga baada ya kumalizika kwa mchezo wao wa fainali dhidi yao na TRA katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi (SHIMUTA).

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Shule ya Sekondari Popatlaly, TRA iliibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Luago alisema tayari wameanza maandalizi ya kufanya uwekezaji huo na kwamba watawekeza kwenye viwanja vya mpira wa miguu, pete na kikapu, huku wakihakikisha watumishi wanapata nafasi ya kucheza michezo hiyo na mingine ili kuimarisha afya zao.

Kuhusu mechi hiyo dhidi ya TRA, alisema licha ya timu yao kupambana vilivyo kuhakikisha wanapata ubingwa, lakini hawakubahatika huku akieleza matarajio yao ni kuongeza nguvu maeneo ambayo yalikuwa na udhaifu ili mashindano yajayo wafanye vizuri.

"Mikakati ni kumsapoti Rais Dk. Samia Suluhu, katika kukuza na kuendeleza michezo ambayo ipo kwenye taasisi zetu kwa ajili ya kuweka afya zetu sawa," alisema.

Alisema katika mashindano hayo kiuhalisi hawakuwa na mategemeo kama wangefika hatua ndefu kama hiyo, hivyo ni matarajio yao wataenda kuongeza nguvu kwenye madhaifu ili wakati ujao waweze kufanya vizuri.

Luoga alisema wataendelea kumsapoti Rais Samia katika kukuza michezo ili kuhakikisha watumishi wanakuwa na afya bora na kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza na mkakati uliopo ni kufanyia kazi miongozo ambayo serikali imeitoa kuhakikisha michezo ina kuwapo kwenye maeneo yao ya ya kazi.

Awali, Mratibu wa Timu ya TFS, Marcel Bitulo, alisema ni mara ya pili wanashiriki kwenye mashindano hayo na mwaka huu wamepambana mpaka wakafikia hatua ya fainali huku akieleza makosa madogo madogo ndiyo yaliyosababisha kupata kipigo hicho.

"Binafsi nawashukuru viongozi wangu, wametutia moyo na timu kuweza kufika hapo ilipo, tunaendelea kujipanga na ukiangalia malengo yetu yametimia kwa asilimia 90 kwa ushiriki na kufika fainali," alisema Bitulo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### DELAP ASAKWA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Ipswich, Liam Delap mwenye umri wa miaka 21, anasakwa na Chelsea baada ya klabu hiyo kusitisha mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Newcastle United, Alexander Isak, 25. ***(Mail)***

#### ARSENAL YAKOMAA NA ISAK

ARSENAL huenda wakajaribu kumshawishi Alexander Isak kuhamia Uwanja wa Emirates Januari kwa ofa ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Give Me Sport)***

#### NKUNKU HANA FURAHA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Christopher Nkunku, hana furaha kutokana na kukosa muda wa kuchezea Chelsea, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hana mpango wa kuondoka Stamford Bridge kwa sasa. ***(Athletic)***

#### ZUBIMENDI ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya jaribio la pili la kumnunua kiungo wa Real Sociedad, Martin Zubimendi mwenye miaka 25 Januari, lakini watakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania. ***(Team Talk)***

#### WAFUATILIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inawafuatilia mshambuliaji wa Lyon, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 21, na mchezaji wa Kimataifa wa Canada, Jonathan David David (24), wa Lille wakati wakitathmini uwezekano wa kumnunua kiungo mshambuliaji Januari. ***(The I)***

#### ZIRKZEE HAKIELEWEKI

WAKUU wa Manchester United wana mashaka na mchezo wa mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye miaka 23, tangu walipomnunua kwa pauni milioni 36.5 kutoka Bologna msimu wa majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

#### GOMES ATAJWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ina matumaini ya kuwashinda Manchester United na Newcastle United katika mbio za kuinasa saini kiungo wa kati wa Lille na England, Angel Gomes, 24. ***(GiveMeSport)***

#### YAMAL MIAKA SITA

WINGA wa Hispania, Lamine Yamal mwenye miaka 17, amekubali kusaini mkataba mpya wa miaka sita katika Klabu ya Barcelona atakapofikisha umri wa miaka 18. ***(El Chiringuito TV, via Football Espana)***

#### BELLINGHAM KUBAKISHWA

KOCHA Mkuu wa Sunderland, Regis Le Bris, anataka viungo wa kati wa England, Jobe Bellingham mwenye miaka 19, na Chris Rigg (17), kusalia kukipiga Uwanja wa Of Light. ***(Sunderland Echo)***

#### BECKER NA GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray inamfuatilia mlinda mlango wa Liverpool na Brazil, Alisson Becker mwenye miaka 32, huku wakimtafuta atakayechukua nafasi ya Fernando Muslera (38), mwishoni mwa msimu huu. ***(Sabah)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# AMORIM: UNITED LAZIMA IANZE KUTESEKA KWANZA

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesema Manchester United italazimika "kuteseka kwa muda mrefu" kabla ya mbinu zake kusaidia klabu hiyo kufurahia mafanikio tena baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Ipswich Town Jumapili na ikamnyima kocha huyo ushindi katika mchezo wake wa kwanza kuiongoza timu hiyo.

**Bao la Marcus Rashford baada ya sekunde 81 liliipa United ndoto ya kupata ushindi, lakini Omari Hutchinson akakisawazishia kikosi hicho cha kocha Kieran McKenna.**

Licha ya kuwa na chini ya wiki moja kufanya kazi na kikosi chake kipya kwenye uwanja wa mazoezi, kocha huyo wa zamani wa Sporting CP alitumia mfumo wa 3-4-2-1 na kusema ilisababisha wachezaji wake kufikiria kupita kiasi uchezaji wao.

**●●● Tutateseka kwa muda mrefu na tutajaribu kushinda michezo, najua inakatisha tamaa, lakini...**

Lakini Amorim alisisitiza kuwa ataendelea kuwa mwaminifu kwa kanuni zake, ingawa alisema itasababisha mateso zaidi hadi mbinu zake zizae matunda.

"Najua inakatisha tamaa kwa mashabiki, lakini tunabadilika sana katika wakati huu na michezo mingi," alisema Amorim akiwaambia waandishi wa habari.

"Tutateseka kwa muda mrefu na tutajaribu kushinda michezo, lakini hii itachukua muda.

"Lazima tushinde michezo, lakini tunaweza kupoteza, kwa hiyo nadhani lazima tuelewe hilo na tufikirie na kuwa na ukweli kwamba watu hawa walikuwa na siku mbili za kufanya mazoezi ili kubadilika sana.

"Ni ngumu kwa wachezaji ndani ya siku tatu kustahimili kila kitu, lakini tunasahau wazo jipya. Nadhani ndio maana nilithe letwa hapa katikati ya msimu na tunajaribu kukabiliana na mambo ambayo wamezoea kufanya chini ya Erik ten Hag.

# ANCELOTTI: MBAPPE ATAIMARIKA ZAIDI UPANDE WA KUSHOTO




**BUTARQUE,** Hispania

CARLO Ancelotti amesifu uchezaji wa Kylian Mbappe baada ya fowadi huyo wa Real Madrid kufunga akicheza katika nafasi ya upande wa kushoto kwenye ushindi wao wa mabao 3-0 dhidi ya Leganes kwenye LaLiga Jumapili.

Mbappe aliiweka Madrid mbele dakika ya 43 huko Butarque, akiunganisha pasi ya Vinicius Junior kabla ya Federico Valverde na Jude Bellingham kila mnoja kufunga bao na kuwawezesha kupata pointi tatu.

Lilikuwa bao la kwanza kwa Mbappe baada ya kubadilishana nafasi na Vinicius, akianzia upande wa kushoto.

"Ulikuwa mchezo mzuri mwanzo hadi mwisho," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Timu ilikuwa imara na yenye umakini. Tulibadilisha nafasi za washambuliaji kidogo, Mbappe akiwa pembeni alifanya vizuri.

"Vinicius alifanya vizuri pia akiwa kati. Tulifungua ukurasa wa mabao, na baada ya hapo timu ilidhibiti mchezo vizuri."

Madrid ilikabiliwa na ukosoaji kwa uchezaji wake katika wiki za hivi karibuni, na kucheza mechi nne bila kupata bao.

"Nilianza katika nafasi tofauti na katika michezo ya hivi majuzi," alisema Mbappe baada ya mchezo.

"Lakini kama nilivyosema siku ya kwanza kufika hapa naweza kucheza katika nafasi tofauti, leo (juzi) ilikuwa tofauti na pengine katika mchezo unaofuata itakuwa tofauti, nipo tayari kuisaidia timu. Ni hadithi ya maisha yangu. Naweza kucheza kulia, kushoto na kati. Ninachotaka kufanya ni kucheza vizuri, kusaidia timu na kufunga mabao."

Baada ya mchezo huo, Ancelotti alitoa sababu zake za kubadili, akiongeza sehemu bora zaidi juu ya ufanisi na matokeo yake ni kuongezeka kwa ushirikiano kati ya nyota wake wawili.

"Nadhani Mbappe amezoea zaidi kucheza upande wa kushoto," alisema Ancelotti.

"Leo (juzi) hiyo ilikuwa bora kwa timu, na kwake pia. Kwa nje inachosha zaidi, na Vini alikuwa amerejea kutoka kwenye jukumu la kimataifa Alhamisi.

# Fernandez atafutiwa dawa Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Enzo Maresca, amekiri kuwa anamhimiza Enzo Fernandez kuingia kwenye eneo la hatari la wapinzani mara nyingi zaidi ili kuwa tishio zaidi.

Kiungo huyo wa kati wa Argentina, hajahakikishiwa nafasi katika kikosi cha kwanza msimu huu, akipambana na Moises Caicedo na Romeo Lavia kuwa mmoja wa viungo wawili wa kati wa Chelsea.

Na Maresca alifichua kuwa anajaribu kurekebisha jukumu la kinda huyo wa miaka 23 ili kumfanya azidi kupata nafasi zaidi uwanjani.

"Ninajaribu kumshawishi Enzo kucheza kama nilivyofanya mwaka jana nikiwa na Ndidi na Kiernan, kwamba viungo washambuliaji wanatakiwa kufika kwenye eneo la hatari," alisema.

"Kwangu mimi anafanya vizuri sana. Nimesema mara nyingi, tangu tumeanza, anafanya kazi kwa bidii. Anafanya bidii kuelewa jinsi tunavyotaka kucheza."

"Wakati mwingine tunamtumia kama kiungo wa kati. Wakati mwingine tunamtumia kushambulia."



# *Slot apagawa na mabao ya Mo Salah*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, amesifu timu yake kwa kurejea kwa nguvu kipindi cha pili katika ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Southampton wakati viongozi hao wa Ligi Kuu England walipokuwa katika hatari ya kupoteza kwa timu ya mkiani kabla ya Mohamed Salah kuwaokoa, Jumapili.

Liverpool walipata bao la kwanza kutokana na makosa ya Southampton, lakini walishindwa kutumia vema kipindi cha kwanza kabla ya wenyeji kupata bao la kushtukiza na kufanya matokeo kuwa 2-1.

Lakini mabao mawili ya Salah yaliwezesha Liverpool kupata pointi zote tatu na kuendelea kukaa kileleni.

"Kipindi cha pili niliona nguvu niliyokuwa nikiitafuta katika kipindi cha kwanza. Southampton inafanya iwe ngumu kwa timu nyingi, ikiwa ni pamoja na timu za juu, na walifanya iwe ngumu leo (juzi), ingawa tulitawala mchezo kabisa," alisema Slot akiiambia Sky Sports. .

"Hakukuwa na uharaka wa kutosha kufika kwenye eneo la hatari katika kipindi cha kwanza, tulibaki tu na mpira badala ya kushambulia. Ingawa tulikuwa nyuma katika kipindi cha pili tulionesha uharaka na nguvu zaidi.

"Hiyo ilisababisha kupata nafasi nyingi na mwishowe mabao mawili. Ni ngumu kutengeneza nafasi dhidi ya mfumo wa 4-5-1.

Mabao mawili ya Salah yalimfanya kufikisha mabao 10 ya ligi msimu huu - mawili nyuma ya mfungaji bora Erling Haaland - na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri amefunga mabao sita katika mechi zake tano zilizopita za ligi.

Slot sasa ameshinda mechi 10 kati ya 12 za ligi, lakini bila shaka anaingia katika wiki yake ngumu zaidi kufikia watakapoikaribisha Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano ikifuatiwa na Manchester City Jumapili ijayo.

HABARI MICHEZO

## Kagoma arejea Simba kuivaa Bravo do Maquis

INATOKA UK. 24

zoezi ya kikosi cha Timu ya Taifa ya Zambia, ilipokuwa ikijiandaa na michezo yake ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), na kulazimika kurejea nchini kwa ajili ya matibabu.

Kocha wa Simba, Fadlu amesema kwa sasa yupo kwenye hatua za mwisho za maandalizi ya mchezo huo, ambao alisema utakuwa mgumu, lakini akitaka ushindi wa mabao mengi ili kujiweka vizuri kwenye kundi hilo na kwa michezo inayofauta.

"Ni kundi gumu, tunatakiwa kwanza tuwe na njaa ya kupata ushindi nyumbani, kama tukipata nafasi tuwe tunazitumia kupata mabao mengi ambayo huko mbele yanaweza kutuvusha. Tunawaomba mashabiki wetu waje kwa wingi kutushangilia na kuwasukuma wachezaji ili wapate morali ya kucheza kwa nguvu na kupambana," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini akiwa kwenye msimu wa kwanza kuifundisha timu hiyo.

## Ramovic ataja mfumo Yanga

INATOKA UK. 24

2-1, hivyo kushindwa kutinga hatua ya makundi msimu huo.

Msimu uliopita ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi na kutolewa kwenye hatua ya robo fainali kwa mikwaju ya penalti 3-2 dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, mechi iliyochezwa Sauzi, Aprili 5, mwaka huu.

Timu hizo zililazimika kupigiana mikwaju ya penalti baada ya kutoka suluhu mara mbili, mchezo wa kwanza ukichezwa nchini, Machi 30, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa Al Hilal, Florent Ibenge, alisema amejiandaa na mchezo wa leo na wamekuja kushinda na si kupoteza mechi.

"Tumekuja tumejiandaa, tumeitazama Yanga na kuichambua kwa kina, lakini ghafla wakabadilik kocha, nina imani mechi itakuwa ngumu sababu bado hatujajua na hatujaona mbinu za kocha mpya wa Yanga ila tumejiandaa kwa asilimia kubwa wachezaji wangu wako tayari kupambana.

"Yanga ina wachezaji wazuri kama Maxi Nzengeli, Pacome Zouzoua, na Stephane Aziz Ki, ni ngumu kuzuia Yanga wasipate bao, lakini tumekuja kupambana nao, kazi yetu kubwa ni kuwazuia wachezaji hao na kusaka ushindi," alisema Mkongomani huyo.

# TABORA UNITED, SINGIDA BLACK STARS ZAKABANA KOO LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WENYEJI Tabora United wamelazimika kufunga mabao mawili ili kuweza kupata sare ya 2-2 dhidi ya Singida Black Stars katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa jana asubuhi, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

**Mechi ililazimika kuchezwa jana badala ya juzi, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha kwenye mikoa ya Tabora na Mwanza, hivyo kusababisha mchezo huo huo kuahirishwa.**

Mechi hiyo iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi wa soka kutokana na Tabora United kuifunga Yanga mabao 3-1 katika mchezo wao wa mwisho uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Novemba 7, mwaka huu, ilijikuta ikipachikwa bao la kwanza dakika ya 16 ya mchezo likiwekwa wavuni na straika hatari wa Singida Black Stars, raia wa Kenya, Elvis Rupia likiwa ni la nne kwake kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Wakati bado Tabora United wakishangaa, beki wa kati raia wa Ivory Coastal, Antony Tra Bi Tra, aliipatia Singida bao la pili dakika ya 32, likiwa pia ni lake la pili kufunga msimu huu.

Sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko, winga wa zamani wa Yanga, raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne aliipatia Tabora United bao la kwanza lililowarudisha mchezoni wachezaji wa timu hiyo.

Hatimaye, Mkongomani, Hiritier Makambo, straika wa zamani wa Yanga, alisawazishia Tabora United bao dakika ya 49, na matokeo hayo yakadumu hadi zilipomalizika dakika 90 za mchezo.

Kwa Yacouba ni bao la tatu kwake msimu huu, huku Makambo likiwa la pili kufunga mpaka sasa.

Sare hiyo inaifanya Singida Black Stars kufikisha pointi 24 sawa na Yanga pamoja na Azam FC, lakini uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa unaifanya ibaki pale pale kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa ligi hiyo.

Azam FC ipo nafasi ya pili ikiwa sawa na Azam kwa pointi na mabao 14 ya kufunga, lakini imeruhusu mabao matatu, huku Wanajangwani wakiruhusu manne na kukaa nafasi ya tatu.

Singida, imefunga mabao 15, moja zaidi kuliko Azam na Yanga, lakini imeruhusu mabao sita kwenye wavu wake.

Tabora United imefikisha pointi 17, ikiwa nafasi ya sita ya msimamo, kwa michezo 12 iliyocheza mpaka sasa.



PAMBANA...

Wachezaji wa timu ya Gongo la mboto (jezi za bluu), wakimiliki mpira dhidi ya Kitunda FC katika mchezo wa kuwania kupanda Ligi Daraja la Tatu, uliopigwa Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *KMKM yazidi kupoteza matumaini ubingwa*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MATUMAINI ya ubingwa kwa timu ya KMKM SC yameendelea kuingia doa baada ya kupokea kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Mlandege FC katika mchezo wa 12 wa Ligi Kuu Zanzibar.

Mchezo huo uliovuta mashabiki wengi uwanjani ulichezwa juzi, Jumapili katika dimba la Mau A majira ya saa kumi za alasiri.

KMKM imeendelea kupata matokeo mabaya karibu michezo minne mfululizo jambo ambalo mashabiki wake wameanza kupoteza matumaini ya mbio za ubingwa msimu huu ingawa bado ni mapema.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu katika dakika zote 90.

Alisema tangu hapo awali alicheza kwa kujihami na kujilinda zaidi kwa kuwa aliwafahamu wapinzani wao wana wachezaji machachari.

Alisema timu yake ilicheza vizuri, lakini makosa madogo ya safu yake ya ulinzi ndiyo yaliyowapa wapinzani wao bao la pili.

Alisema bao la pili lilitokana na mpira uliopigwa nje ya boksi na kutinga moja kwa moja wavuni jambo ambalo wachezaji wake wangekuwa makini na mpigaji wa mpira huo wangefanikiwa kuzuia shambulizi hilo.

"Tulicheza na timu ambayo ina wachezaji machachari na hodari, kuna wakati tulikosa umakini kutokana na kasi ya mchezo jinsi ulivyokuwa, lakini bahati ilikuwa yao wametufunga," alisema.

Aidha, alisema bado ni mapema kwa mashabiki wa timu hiyo kupoteza matumaini ya kutwaa ubingwa kwani wanayo nafasi ya kurekebisha makosa yaliyopo na timu ikarudi kufanya vizuri.

Kwa matokeo hayo Mlandege FC imekwea kileleni mwa msimamo wa ligi kwa kufikisha alama 24, nafasi ya pili ikishikiliwa na mafunzo yenye alama 23 ambayo bado hajacheza mchezo wake wa 12.

Michezo

Jumanne Novemba 26, 2024

Nipashe



Fernandez atafutiwa dawa Chelsea UKURASA 22

# Ramovic ataja mfumo Yanga kuimaliza Al Hilal

●●● Asema leo ni 'mpera mpera' mwanzo mwisho, Ibenge naye awataja Nzengeli, Pacome na Aziz Ki kuwa...

**Na Adam Fungamwangwo**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, leo saa 10:00 jioni watashuka kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam kucheza mechi ya raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, huku Kocha Mkuu, Sead Ramovic, akisema hatowapa wapinzani nafasi ya kupumua.

**Akizungumza jana kuelekea kwenye mchezo huo wa Kundi A, kocha huyo ambaye itakuwa ni mechi yake ya kwanza kuiongoza Yanga, alisema katika mchezo huo atataka kutambulisha aina yake ya uchezaji ambayo yeye huihusudu sana, nayo ni mpira wa uthubutu, wenye nishati kubwa, kushambulia, kushinikiza mpinzani muda wote wakati hawana mpira na kutomruhusu kupumua kwa kushambulia mfululizo.**

Alisema kutokana na ubora wa wachezaji wake, anategemea watacheza soka safi na la kuburudisha na hatimaye kuibuka na ushindi katika mchezo huo.

Hata hivyo, alisema itachukua muda kidogo kufika kwenye ubora huo kwa asilimia 100 kwani ndiyo kwanza ameichukua timu na inahitaji muda kufikia viwango vya hali ya juu ya aina hiyo ya soka.

"Staili yangu kimchezo ni ya tofauti kidogo, napenda mpira wenye uthubutu na nishati kubwa kushambulia, kushinikiza wapinzani muda wote katika maeneo yote tusipokuwa na mpira na kutoruhusu mpinzani kupumua. Staili hii inahitaji kazi kubwa na utimamu wa mwili kuikamilisha inachukua muda kufikia ubora huo, hata hivyo sina shaka tutafikia hatua hii kutokana na ubora wa wachezaji tulionao.

"Yanga yangu itakuwa yakuburudisha mno, hilo naahidi, katika mchezo huu tunaonesha kile ambacho tumeshaanza kukifanyia kazi," alisema Ramovic ambaye amechukua kikosi hicho baada ya kufutwa kazi kwa Miguel Gamondi.

Yanga inakwenda kucheza na Al Hilal, ikikumbuka kilichotokea Oktoba 8, 2022 kwenye uwanja huo ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 katika mchezo wa raundi ya kwanza wa ligi hiyo, na ule wa marudiano uliochezwa nchini Sudan, Oktoba 16, mwaka huo ilifungwa bao 1-0 na kutolewa kwa jumla ya mabao

INAENDELEA UKURASA 23



Kiungo wa Yanga, Clautos Chama, akitoka mazoezini jana. Leo atakuwa na kazi pevu ya kuisaidia timu yake dhidi ya Al Hilal kwenye mechi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. **MPIGAPICHA WETU**

# Kagoma arejea Simba kuivaa Bravo do Maquis

**Na Adam Fungamwangwo**

HABARI njema kwa wanachama na mashabiki wa Simba ni kwamba, kiungo mkabaji asilia wa timu hiyo, Yusuph Kagoma, amepona na amerejea mazoezini na wenzake kwa ajili ya mchezo wa kesho dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola.

Mchezo huo wa raundi ya kwanza, hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho, unaotarajiwa kupigwa kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kagoma ameonekana kwenye Uwanja wa Mo Arena Bunju Dar es Salaam, akifanya mazoezi na wachezaji wenzake kuelekea kwenye mchezo huo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amekiri jana kuwa mchezaji huyo amepona na yupo fiti kwa ajili ya mchezo huo, kilichobaki ni maamuzi ya Kocha Mkuu, Fadlu Davids.

"Maandalizi yanakwenda vizuri, mwalimu Fadlu anaendelea kukinoa kikosi chake kuelekea kwenye mchezo wetu na kila kitu kiko sawa sawa, hakuna majeruhi yeyote kwa sasa, wote wameshapona, Abdurazack Hamza aliingia kipindi cha pili katika mchezo wetu uliopita dhidi ya Pamba, Joshua Mutale naye ameshapona, Kagoma tangu kikosi kiliporejea mazoezini amekuwa na wenzake kwa ajili ya kupata utimamu wa mwili na yupo tayari kwa mchezo," alisema Ahmed.

Kagoma na Hamza, hawakuonekana uwanjani tangu Oktoba 19, mwaka huu, walipopata majeraha kwenye mchezo dhidi ya Yanga uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hata hivyo, Hamza alionekana akiingia katikati ya kipindi cha pili, Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, timu hiyo ilipocheza dhidi ya Pamba Jiji na kushinda bao 1-0.

Mutale aliumia kwenye ma-

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042